ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Pili – Tarehe 24 Machi, 2011

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya Mikataba ya Amana ya Mali zinazohamishika pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Abdalla Ali (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala):
Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Miakataba ya Amana ya Maji zinazohamishika pamoja na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 81

Maafa Yaliyosababishwa na Upepo Mkali

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza**:-**

Siku ya Jumatato 09/02/2011, Kisiwa cha Unguja katika maeneo ya mjini na vijijini, kilikumbwa na upepo mkali uliopelekea maafa makubwa. Upepo huu pia uliendelea kisiwani Pemba kwa siku nne baadae, ingawa kwa kasi ndogo. Kwa kuwa Mamlaka ya Hali ya Hewa ina wajibu wa kutoa taarifa na tahadhari kwa umma kabla na baada ya kutokea kwa majanga yanayosababishwa na upepo, jua, mvua, bahari na mengineyo.

(a) Je, Mhe. Waziri, kwa nini Mamlaka ya Hali ya Hewa haikutoa taarifa au tahadhari ya ukubwa wa upepo huo kabla siku ya tukio.

(b) Je, upepo huo ulivuma kutoka muelekeo gani na ulikuwa na ukubwa wa kiasi gani.

(c) Ni nyumba ngapi za wananchi zilizopatwa na maafa.

(d) Kwa kuwa wakati wa tukio hilo, madereva walikimbia kwa mwendo wa kasi na kusababisha ajali. Mfano gari ya *Toyota Prado* lililowagonga na kusababisha vifo vya watoto wawili, katika maeneo ya Welezo. Je, Serikali imefuatilia vipi tukio hilo na kuwasaidia waathirika wa ajali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, janga ni kitendo chenye uwezo wa kusababisha matokeo yanayoleta madhara kwa maisha ya binaadamu, mali zao na mazingira yanayowazunguka. Athari za janga ndizo zinazosababisha maafa. Maafa ni tukio kubwa linalotokea na jamii kushindwa kuendelea na utaratibu mzima wa kazi zao, tukio ambalo husababisha vifo, mateso au upotevu wa mali na uharibifu wa miundombinu na mazingra n.k. Uharibifu huo unazidi uwezo wa jamii katika kukabiliana na maafa hayo. Kwa hivyo tukio la upepo uliotokea tarehe 09/02/2011 na kuleta hasara kwa jamii ilikuwa ni janga. Serikali kwa kushirikiana na wananchi ilichukua hatua mbali mbali kukabiliana na hali hiyo, tuna mshukuru Mwenyezi Mungu hali sasa ni shwari.

Mhe. Spika, sasa naomba kulijibu swali kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa kanda ya Zanzibar ina utaratibu kupitia vipindi vyake vya Televisheni Zanzibar na Sauti ya Tanzania Zanzibar kutoa utabiri wa hali ya hewa nchini. Hata hivyo siku ya tarehe 08/02/2011 indhari ya kutokea mvua itakayoambatana na ngurumo za radi ilitolewa. Aidha, tahadhari ya muelekeo wa ongezeko la kasi ya upepo kwa visiwa vyote vya Unguja na Pemba hadi tarehe 19/02/2011 ilitolewa. Pia Mamlaka iliwataka watumiaji wa vyombo vya baharini kuchukua tahadhari katika kipindi chote hicho.

(b) Mhe. Spika, upepo huo ulivuma kutoka Kaskazini hadi Kaskazini Mashariki kwa kasi ya kilomita kumi hadi ishirini kwa saa na baadae uliongezeka na kufikia kilomita thalathini na tano kwa saa.

(c) Mhe. Spika, kutokana na taarifa ya Kamati zetu za Maafa Wilayani jumla ya nyumba 216 ndizo zilizoathirika kutokana na janga hilo, kati

ya hizo nyumba 206 ni za watu binafsi na majengo 10 ni mali ya JKU katika Kambi ya Bambi. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole wale wote walioathirika na janga hili.

(d) Mhe. Spika, ni kawaida kuwa yanapotokea majanga mbali mbali watu hupatwa na mishituko na taharuki hivyo kila mmoja huwa anatafuta namna ya kujinusuru. Kuhusu ajali iliyotokea Welezo taasisi zinazohusika na ajali za barabarani zilichukua hatua kwa mujibu wa taratibu zao. Hata hivyo, ofisi yangu itaendelea kufuatilia suala hili ili kuona haki inatendeka.

Mhe. Spika, naomba kutoa wito kwa madereva na watumiaji wengine wa barabara kuchukua tahadhari zaidi katika matumizi ya barabara hasa katika nyakati za mvua zinazoambatana na upepo mkali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja.

a) Kwa kuwa sambamba na upepo ule zipo taarifa kwamba vijiji vya maeneo ya Wilaya ya Kati vilipata na kunyeshewa na mvua ya mawe. Je, hili ni kweli na kama ni kweli kulikuwa na athari gani.

b) Kwa kuwa siku ile watoto wawili wanafunzi wa familia moja walifariki pale Welezo kwa sababu ya mbio nyingi zilizosababishwa na upepo na mvua ile, kupitia Idara ya Maafa wizara yako iliwasaidia nini wafiwa wa watoto wale.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais:

a) Kuhusu suala la mvua ya mawe Wizara yangu haina taarifa hizo za mvua za mawe.

b) Kuhusu wanafunzi wawili ambao wamepata ajali Welezo bado wizara yangu inafuatilia suala hili ili kujua kwamba ajali ile chanzo chake ni upepo ama ni ajali ya kawaida inayoweza kutokea barabarani. Kwa sasa bado tunawasiliana na Polisi ili kujua ukweli halisi wa jambo hilo mara tutakapopata taarifa kamili nitamjibu Mheshimiwa kwa maandishi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja.

a) Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kuwa vyombo vya mamlaka vya hali ya hewa vimepitwa na wakati.

b) Pili mpaka sasa hivi katika nyumba ambazo zimepatwa na maafa nyumba ngapi ambazo tayari mmeshaanza kuzilipa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kuhusu vyombo vya hali ya hewa kuwa vimepitwa na wakati ni vyema tukaelewa kwamba kwa sasa vyombo vyetu hivi vinafanya kazi vizuri, inawezekana kwamba sio vya kisasa sana kama ambavyo tungetarajia iwe lakini vinasaidia sana katika shughuli zake. Kwa hivyo namuomba Mheshimiwa avute subra huku tukiwasiliana na wahusika na kuhakikisha kwamba Zanzibar inapata vyombo vya kisasa zaidi vya kazi vya hali ya hewa.

Kuhusu malipo ya nyumba kazi yetu ya mwanzo tulifanya tathmini na tathmini iliyoonyesha ni kama ifuatavyo.

Uharibifu uliotokea katika nyumba za JKU Bambi una thamani ya Sh. 74,585,129/=. Katika Wilaya ya Mjini uharibifu uliotokea ni wa thamani ya Shs. 32,053,500/=.
Katika Wilaya ya Magharibi ni Shs. 40,4300,375/=.

Kwa sasa hali ya Wizara yangu haina uwezo wa kuweza kulimaliza tatizo hili pamoja hasa kutokana na hali yetu kuwa ni ngumu kwa sana, tunawaomba wananchi na wafadhili wengine wajitokeze kusaidia wenzao ili waepukane na janga hili ambalo limewakuta, hali yetu kwa sasa hatujaweza kusaidia nyumba yoyote ile ambayo imepata taathira hizi.

Nam. 97

Kuondoshwa Makontena Sehemu ya Darajani

Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza**:-**

Mhe. Spika, eneo la Darajani limekuwa likitumiwa vibaya na wafanyabiashara na wasio wafanyabiashara katika vitendo mbali mbali vya kihalifu kama vile uuzaji wa mihadharati, wizi wa mifukoni, utapeli, udhalilishaji kijinsia, uuzwaji wa bidhaa zilizokwisha muda na usumbufu kwa wanafunzi wa skuli ya Darajani na Vikokotoni.

Aidha, lengo la Serikali katika eneo lile ni kulifanya kuwa ukanda wa kijani *(Green Belt)* na sio biashara kama ilivyo hivi sasa. Mwaka 2007 Serikali iliwaondoa wafanya biashara wadogo wadogo na kuwapeleka Saateni, lakini

wafanyabiashara hao walirudi kwa kisingizio kuwa watakwenda Saateni endapo makontena ya Darajani yataondoka.

(a) Je, kuna sababu gani inayokwamisha kuondolewa kwa makontena ya Darajani ili kuweza kuliacha eneo hilo kuwa wazi kwa ajili ya bustani na maegesho ya magari kama ilivyokusudiwa na Serikali.

(b) Ni nini mpango mpya wa Serikali katika eneo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 97 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, sababu inayokwamisha kuyaondoa makontena pale Darajani ni suala suala la baadhi ya wenye makontena kutokufahamu hasa nini madhumuni ya kupaendeleza pale pahala, sasa baada ya wao kutokufahamu wakafanya mgomo baridi na mgomo wenyewe wa kwenda Mahakamani kuweka pingamizi kwamba makontena yale yasiondoshwe hapo ndipo tulipokwama. Kesi hiyo tayari iko Mahakamani kwa mara ya kwanza kesi ilisikilizwa tarehe 3/03/2011 ambapo ilitajwa na kuagizwa watu wa Baraza la Manispaa wapeleke vielelezo na vielelezo vilipelekwa tarehe 17/3/2011 na umepigwa tarehe tena hadi tarehe 29/03/2011 ambapo kesi yao itatajwa tena.

Mimi nimefurahi sana na Mhe. Ali Salum Haji kwa kutoa maelezo yeye mwenyewe mazuri kabisa na akafahamu hasa nini madhumuni ya hapa Darajani, pale hapakukusudiwa kumkwamisha yeyote wala kumpendelea mtu yeyote.

(b) Mhe. Spika, kuna mpango wa muda mrefu wa kupaendeleza pahali pale na kupafanya kama ni eneo lililo wazi kwa ajili ya bustani na maegesho ya magari, yaani *green belt area* kwa mujibu wa mpango wa hifadhi ya Mji Mkongwe. Tayari mpango huu tunashukuru umepata ufadhili mzuri kabisa wa Benki ya Dunia ambao watachangia awamu ya pili wa mradi ya michirizi zaidi ya shilingi bilioni tatu.

Kwa hivyo mimi nawaomba sana wafanya biashara wa eneo lile wakubaliane na serikali yao katika kupaendeleza pahali pale, sote tunapakumbuka Darajani ilivyokuwa wakati huo likiitwa daraja, baadae pakaendelezwa pakafukiwa tukumbuke soko la zamani lilikuwa vipi, pakaendelezwa tena mpaka palivyo leo. Kwa hivyo

serikali ina mpango tena na ramani tumeweka pale ya kuwaelimisha. Mimi nawasihi hao waliokwenda huko Mahakamani waondoe kesi yao twende na mpango wetu wa serikali na wataona matunda yake pahali pale.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa serikali mambo yake ni ya mpango na ikiwa ni ya mpango huwa inajulikana muda mrefu, hutokezea je hata ikawa wakati wa utekelezaji wa shughuli zake za serikali ikawa ndio kunaanza mikwaruzano na wananchi wake, ni sababu zipi za msingi zinazopelekea kukwaruzana na wananchi wake wakati serikali mambo yake hupangwa kwa mipango na bajeti na kila aina ya utayarishaji.

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika**, s**erikali ina mipango yote ya muda mrefu na muda mfupi yeye ni msomi mzuri tu anafahamu wala sihitaji kumuelimisha hayo, lakini kwa suala la Darajani ni suala la muda mrefu na ukweli serikali haikupendelea kutumia nguvu inapenda sana kwa wananchi wake twende vizuri, tunasihiane, tuwafahamishe wafahamu. Naamini wafanya biashara wa Darajani wengine wamefahamu na wameshaamua kuondoka pale sasa hao wengine bado hawajafahamu lakini tutaendelea kuwafahamisha taratibu waweze kuhama na kuhamia pahala ambapo pameshatengwa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri nani aliyewaruhusu wananchi kuweka makontena pale, na sasa hivi ni nani anayetaka kuwahamisha kutoka makontena pale. Kwa sababu wananchi wameshaweka makontena na muda umeshapita leo hii wanataka kuondolewa, ni nani hasa aliyeruhusu kuweka makontena pale na nani anayetaka kuhamisha wanachi sehemu ile pale.

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, walioruhusu pale ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya biashara zao kwa wakati ule sio mtu binafsi. Sasa wakati umefika Serikali hiyo hiyo inataka kupaendeleza mahali pale, kwa hivyo tunawaka wananchi wale waondoke. *(Makofi).*

Nam. 15

Chuo cha Uongozi wa Fedha Kukabiliwa na Changamoto Mbalimbali

Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Aliuliza**:-**

Tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha Chuo cha Uongozi wa Fedha kilichopo Chwaka na kuweza kutoa wataalamu wengi wa fedha. Hazina hiyo hutumiwa na vitengo na taasisi mbali mbali za Serikali na za watu binafsi, lakini bado Chuo hicho kinakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo za ukosefu wa Dahalia, maji safi na salama, usafiri kwa wanafunzi watokao mjini na kadhalika.

Kwa kuwa Chuo hicho ni muhimu sana katika nchi yetu na nchi za jirani, je, wizara ina mikakati gani ya kuondoa matatizo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 15 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliona upo umuhimu mkubwa wa kuanzisha Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sekta ya fedha hapa nchini na duniani kwa ujumla. Chuo hicho kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi kwamba kinazalisha wataalamu wa sekta ya fedha na kinatoa mchango mkubwa wa nguvu kazi kwa taasisi na idara za Serikali pamoja na sekta binafsi.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inaelewa kuwepo kwa changamoto zinazokikabili Chuo hicho. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2011, Serikali imeweza kuzifanyia kazi changamoto hizo kama ifuatavyo:-

- Mhe. Spika, upande wa dakhalia tayari Serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Dakhalia ya wanafunzi.

- Ujenzi huo hadi kukamilika kwake utagharimu jumla ya Shs.3,505,545,879. Kati ya hizo, mkopo wa *ZSSF* ni 1,800,000,000 na mchango wa Serikali ni 1,700,000,000. Ujenzi wa Dakhalia tayari umeanza rasmi katika mwezi wa

Machi, 2011 na unatarajiwa kuchukua muda wa mwaka mmoja hadi kumalizika kwake.

- Kwa upande wa maji safi na salama katika chuo hicho, tatizo hili ni la eneo zima la kujiji cha Chwaka na tayari linajulikana na Wizara inayoshughulikia masuala ya maji.

- Wizara ya Maji kwa kushirikiana na uongozi wa Jimbo la Chwaka inaendelea na mchakato wa kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hili na kupatikana maji safi na salama.

- Upande wa usafiri wa wanafunzi ni kweli tatizo lipo kwa muda mrefu na linatokana na kuongezeka kwa wanafunzi pamoja na Chuo kuwa na gari chache pamoja na kutokuwa na Dakhalia ya wanafunzi, kwa vile ujenzi wa Dakhalia ya wanafunzi umeshaanza ni mategemeo yetu kwamba tatizo la usafiri kwa wanafunzi halitokuwepo tena baada ya kukamilika kwa ujenzi

Nam. 121

Kuadhimishwa Siku ya Kuanza kwa Mwaka wa Kiislami

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Ni dhahiri kuwa Wazanzibari tuliowengi ni Waislamu. Tunakubali pia kuwa Uislamu ni mfumo mzima wa maisha yenye mila zake, desturi zake, hulka zake na sherehe zake. Lakini kama zilivyo mila, desturi, silka na hulka nyengine, mambo haya yanahitaji kutunzwa na kuadhimishwa.

Je, Mhe. Waziri, wizara yako haioni kuwa katika kuzienzi mila, desturi, silka na hulka za Kiislamu kuna haja ya kuadhimisha kuanza kwa mwaka wa Kiislamu na kuifanya siku hiyo iwe ni siku ya mapumziko hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 121 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba Wazanzibari tulio wengi ni Waislamu na pia nakubaliana naye kwamba upo umuhimu wa kuzienzi mila, desturi, na silka za Kiislamu kwa vile ni mfumo mzima wa maisha ya kila siku ya Wazanzibari walio wengi.

Mhe. Spika, Uislamu unazo sikukuu mbili rasmi nazi ni Idd el Ftri na Idd el Hajj. Aidha Mhe. Spika, kwa utukufu wa mazazi ya Mtume Muhammad (SAW), siku hiyo pia inatambuliwa rasmi ni siku ya sikukuu. Tarehe 1 Muharami sio siku rasmi ya serikali lakini serikali kwa kuenzi mila na silka za Kiislamu serikali inaruhusu kufanyika kwa sherehe hizo maeneo yote ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, nakiri ipo haja ya kuliangalia kwa undani zaidi suala hili la sikukuu ya mwezi Mosi Muharram. Kwa hivyo basi Wizara yangu itafanya utafiti kwa kupitia Sheria za Kiislamu, na kwa kutazama Ijtihad za Maulamaa ili tupate kuwa na uwezo wa kuishauri Serikali vizuri na kwa ustawi kuhusu kuifanya siku ya mwezi Mosi Muharram kuwa sikukuu ya Kitaifa. Wizara inaahidi kufanya hivyo kwa kushirkiana na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa sababu hii ndio Wizara hasa inayohusika na sikukuu za Serikali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri mwenyewe amekubali na kusema ipo haja ya kuanzisha mwaka wa Kiislamu au kuazimisha siku ambayo mwaka wa Kiislamu inajulikana.

a) Je, Mhe. Waziri ni utafiti gani tena unaohitajika katika kulitolea uamuzi suala hili la kuadhimisha mwaka huu wa Kiislamu.

b) Muda gani unahitajika kulitolea uamuzi suala hili la kheri na nyeti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo ni kwamba sikukuu hizi za kiserikali ni Afisi ya Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais ndiye anayehusika. Sasa hili suala baada ya kulipata na kutizama kwa uhakika kwamba kuna sikukuu ngapi za Kiislamu ni kama alivyozitaja za Mfungua Mosi, mfunguo tatu na siku kuu ya kuzaliwa Muhammad (SAW).

Sasa kwa kuifanya sikukuu hii ya Muharami kuwa ni sikukuu ya serikali lazima kwanza tutizame na tufanye tafiti ili tutapokubaliana hapo tena ndipo tunaweza kuitangaza kwamba ni sikukuu ya kiserikali, lakini hatuwezi kusema hivi sasa kwamba itachukua siku moja au wiki mbili lazima tutizame utafiti na tukubaliane na wenzetu ili tuweze kuitangaza kama tutakubaliana kama ni sikukuu ya serikali au siyo sikukuu ya serikali.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nashukuru naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Zanzibar inatambua tarehe zote

mbili za kalenda katika redio yake, kuna ugumu gani wa kuitambua siku hii ya Muharam iwe ni siku ya sikukuu kwa nchi yote.

Mhe. Spika: Mheshimiwa labda ueleze zaidi maana majibu umeshatoa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa sababu hizo hizo anazohofia Mhe. Rashid ndio nikasema kwamba Serikali ni lazima ifanye uchunguzi na utafiti baada ya kufanya uchunguzi na utafiti na kupata maelekezo kutoka kwa maulamaa wetu, hapo ndio tunaweza tukasema kwamba kuna umuhimu wa siku hii kuifanya kwamba ni sikukuu ya serikali au hakuna umuhimu. Kwa hivyo hapo ndio tutajua na baadaye ndio serikali itasema kutokana na kwamba kuna umuhimu basi ifanywe kuwa ni sikukuu ya serikali au kutokana na kwamba hakuna umuhimu isifanywe kuwa ni sikukuu ya serikali. Uchunguzi ndio utakaotufanye tujue kwa uhakika.

Nam. 18

Wananchi wa Kawaida Kujiunga na Chuo cha Utawala wa Umma kwa Asilimia Kubwa

Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Aliuliza:-

Chuo cha Utawala wa Umma kimeanzishwa ili kuwapatia fursa za mafunzo Watumishi wa Umma, lakini imebainika kuwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga Chuoni hapo ni wananchi wa kawaida (sio watumishi).

(a) Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zinazopelekea Wizara za Serikali kushindwa kuwapeleka Watumishi wake Chuoni hapo.

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa malengo na dhamira ya uanzishwaji wa Chuo hicho yanafikia.

(c) Kwa kuwa Chuo cha Utawala wa Umma kipo katika mazingira yasiyoridhisha; Serikali ina mikakati gani ya kumaliza ujenzi wa Chuo hicho huko Tunguu hasa tukizingatia kuwa Chuo hukodi majengo ili kuendesha vyema shughuli zake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma kimeanzishwa rasmi mwaka 2007 kwa Sheria Nam. 1 ya mwaka 2007. Sheria hiyo imeweka utaratibu wa uendeshaji wa Chuo pamoja na majukumu yake. Chuo hiki ni moja ya vyuo mbalimbali hapa nchini, vinavyotoa elimu na taaluma mbalimbali kwa Watumishi wa Umma na taasisi binafsi kulingana na kada au mahitaji ya watumishi hao.

Mhe. Spika, kazi za Chuo cha Utumishi wa Umma ni kutoa taaluma kwa wananchi wote isipokuwa mitaala yake mingi inahusu shughuli za kiofisi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali haijashindwa kuwapeleka watumishi wake katika chuo cha Utumishi wa Umma, na Chuo kinaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa serikali kwa mujibu wa mahitaji na aina ya mafunzo. Kuwepo kwa wanafunzi ambao sio watumishi wa serikali ni kwa mujibu wa Sheria ya Chuo cha Utumishi wa Umma kifungu Namba 4(a), ambayo imekipa jukumu la kutoa taaluma katika sekta zote.

(b) Mhe. Spika, serikali ina mpango wa kuimarisha zaidi chuo hiki kitaaluma kwa kujenga jengo jipya eneo la Tunguu, kufundisha walimu na kuweka mazingira bora ya utendaji wa chuoni. Aidha chuo tayari kinatambulika rasmi na wanafunzi wanaofaulu hapo wanaweza kuajiriwa Zanzibar na nje ya Zanzibar bila ya wasiwasi.

(c) Serikali hivi sasa inaendelea na ujenzi wa chuo huko. Tunguu ili kukabiliana na kadhia hiyo ambayo Mhe. Mwakilishi ameieleza.

Nam. 24

Ujenzi wa Visima Unaofanywa na Viongozi

Mhe. Mgeni Hassan Juma – Aliuliza**:-**

Kwa kuwa tatizo la maji limekuwa sugu katika maeneo mengi, viongozi wetu wa Kisiasa wameamua kuchimba visima ili kupunguza ukali wa tatizo hilo.

(a) Je, wizara yako inayo taarifa ya uchimbaji wa visima hivyo.

(b) Je, wizara inachangia vipi katika kuhakikisha kuwa visima hivi vinatoa maji safi na salama.

(c) Je, ni visima vingapi tayari vimeshachimbwa na viongozi wetu hawa katika eneo la Mjini Magharibi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu haina taarifa za uchimbaji wa visima hivyo. Utaratibu Mamlaka ya Maji wa kuchimba visima ni kwa wahusika kuja Mamlaka na kwamba kibali cha kuchimba visima na hatimae kuvifanyia usajili.

(b) Wizara yangu haitaweza kuhakikisha hilo wakati hata taarifa za kuwepo kwake haina na kwa wale wanaotoa taarifa wizara yangu inawapatia dawa maalum ya *chlorine* ili kutia katika maji hayo kwa kuwa vimelea vya maradhi na kuhakikisha kuwa hapo safi na salama.

(c) Kwa kuwa visima hivyo havikusajiliwa Wizara yangu haina takwimu zake hadi sasa.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri kuna taarifa ya kuwa kuna watu wengi wanapeleka maombi ya kuchimba visima lakini maombi yao hayajibiwi. Je, hili ni kweli?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwenye suala zima la uchimbaji wa visima inabidi serikali ichukue tahadhari kubwa. Kwa sababu uchimbaji wa kiholela unaweza kusababisha matatizo makubwa ya kimazingira na kusababisha tatizo kubwa la maji nchini. Hivyo hatua zinachukuliwa ili vibali vitolewe tu kwa pale ambapo mahitaji hayo yatahitajika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa fursa hii kuweza kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri, pamoja na majibu yake mazuri.

Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kuwa hivi sasa visima vingi vimeshachimbwa katika maeneo. Je, kama suala hilo ni kweli kuna utaratibu gani katika Wizara yako ili kuweza kuvisaidia kuokoa ili watu wasipate kuambukizwa na maradhi ya kuharisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyosema awali ni lazima tahadhari zichukuliwe katika kuhakikisha kwamba mazingira yanalindwa na usalama wa nchi yetu unalindwa. Ushauri wake tunauchukua ili tufanye kazi zaidi kwa kufanya tathmini ya visima vilivyochimbwa na ushauri sahihi utolewe ili kulinda mazingira ya nchi yetu.

Mhe. Abadalla Juma Abdalla: Nakushukuru Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri mimi naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mfumko wa uchimbaji visima kiholela unasababishwa na upungufu mkubwa wa maji katika maeneo hayo. Je, ana mpango gani katika wizara yake ili kuhakikisha upatikanaji wa maji unakuwa wa kawaida ili visima hivi visiendelee kuchimbwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la maji, lakini serikali inachukua jitihada mbali mbali kuhakikisha kwamba hali ya maji katika nchi yetu inakuwa nzuri.

Mipango imewekwa ili kuhakikisha kwamba ugawaji wa maji nchini unapatikana. Kwa hivi sasa kwa kusaidiwa msaada wa Japan tumeanza kuhakikisha kwamba maji katika Wilaya ya Mjini Unguja yanaanza kufanikiwa. Hata hivyo, jitihada zitachukuliwa kuhakikisha kwamba maji yanapatikana. Kwa wakati huu tutaendelea kufanya tathmini ya kuona yale maeneo ambayo yatahitaji maji na yatakuwa yanahitaji kuchimbwa kisima basi hatua hizo zitafanywa.

Nam. 47

Gharama za Vifaa vya Michezo

Mhe. Omar Ali Shehe – Aliuliza**:-**

Katika kuelekea kujiunga na Shirikisho la Soka Duniani (*FIFA*), mchezo wa mpira wa miguu Zanzibar, unakabiliwa na changamoto nyingi katika mageuzi ya mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa vilabu na ligi za ndani. Moja kati ya

changamoto hizo ni uwezo wa timu katika kukabiliana na gharama za usajili wa wachezaji na umiliki wa vifaa vya michezo.

(a) Je,kwa kuzingatia bei ya vifaa vya michezo ilivyo hivi sasa, serikali haioni kuwa vilabu vingi vinashindwa kumudu gharama za vifaa hivyo kupelekea kuzorota kwa maendeleo ya vilabu hivyo.

(b) Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na wafanyabiashara ili kupunguza gharama za bei za vifaa vya michezo nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Utalii na Michezo – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam, 47 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika kuelekea kujiunga na Shirikisho la Soka Duniani *(FIFA*), mchezo wa mpira wa miguu duniani Zanzibar unakabiliwa na changamoto nyingi katika mageuzi ya mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa vilabu na ligi za ndani. Moja kati ya changamoto hizo ni uwezo wa timu katika kukubaliana na gharama za usajili wa wachezaji wa upatikanaji wa vifaa vya michezo.

(a) Mhe. Spika, kwa sasa serikali haina mpango wa kushirikiana na wafanyabiashara ili kupunguza gharama za bei za vifaa vya michezo nchini. Wizara kwa vile ndio inayohusika na michezo itashirikiana na Wizara ya Biashara na Wizara ya Fedha kufikiria uwezekano wa kupunguza gharama za bei za vifaa vya michezo nchini.

(b) Ni kweli kuwa bei ya vifaa vya michezo ilivyo sasa ni kubwa mno. Na ni kweli pia kuwa vilabu vingi vinashindwa kumudu gharama za vifaa hivyo. Hali hiyo inapelekea kuzorota kwa maendeleo ya vilabu hivyo. Katika kukabiliana na tatizo hilo, vizara imejipanga kuomba misaada ya vifaa vya michezo kupitia wahisani na wafadhili mbali mbali wakiwemo Wajumbe wa Baraza lako tukufu kupunguzia mzigo vilabu vya michezo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize maswali mawili yafuatayo:-

(a) Kwa kuwa ni kweli kwamba tuna tatizo hilo la kupanga kwa bei za vifaa vya michezo. Je, serikali haioni sababu ya kuandaa mkakati maalum wa kupunguza ushuru kwa ajili ya vifaa hivyo.

(b) Wizara ina mpango gani kwa sababu sasa hivi masuala mengi ya michezo huwa inaendeshwa na wadhamini. Je, serikali ina mpango gani hasa wizara kutafuta wadhamini kwa ajili angalau kuvipatia vilabu vyetu hasa vikubwa vifaa vya michezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli vilabu vingi vinakosa ufadhili na vinakosa na gharama hizo. Lakini wizara kwa kushirikiana na wafanyabiashara watalifuatilia suala hili kulipatia ufumbuzi wa haraka.

Mhe. Spika: Kulikuwa kuna suala la upunguzaji ushuru pamoja na kutafuta wadhamini, serikali ina mpango gani. Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa heshima yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kuhusu gharama za vifaa. Tumo katika mchakato wa kukaa na Wizara ya Fedha ili kupunguza ushuru juu ya masuala ya vifaa vya michezo. Nafikiri tutakaa hivi karibuni tu kwa hivyo hilo halina mjadala.

Mhe. Nassor Salum Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, tatizo la vifaa vya michezo havipo katika timu hizi za vilabu vya kawaida bali vipo hata katika timu yetu ya Taifa *Zanzibar Heroes* pamoja na timu zetu za Taifa za Vijana.

Timu zetu hizi za Taifa zimekuwa ni omba omba katika kutafuta vifaa hivyo vya michezo ya Timu ya Taifa. Je, Wizara ina mpango gani kuhakikisha kwamba timu ya Taifa za Vijana pamoja na timu ya wakubwa *Zanzibar Heroes* inaondokana na hili tatizo la omba omba za vifaa na kuiweka nembo ya Zanzibar katika jezi hizo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nashukuru kwa swali zuri. Kwa kweli hivi sasa wizara tumeshapata wafadhili na mfadhili wa kwanza ni *Future Century* ambaye ndiye atakayeidhamini timu ya Taifa ya Zanzibar Heroes ambaye yeye ndiye atakayechukua dhamana hiyo ya kuipatia vifaa vile vile. Kwa hivyo nafikiri suala la vifaa litakuwa halina mjadala kwa sababu tayari tunae mfadhili na wadhamini tunao. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri. Pamoja na jitihada wanazozifanya za kupunguza gharama ili kupata vifaa kwa bei ya chini. Nataka nimuulize vifaa watakavyohitajia kuvileta ambavyo vya gharama ya chini vitakuwa vimefanywa katika ubora gani. Kwa

sababu vifaa vya michezo na hususan viatu vinatengenezwa katika mazingira ya viwanja vyenye nyasi. Viwanja vingi vya michezo katika nchi yetu hii havipo katika ubora.
Je, kuna njia gani ambayo ataifanya kupata vifaa vyenye ubora ili kuja kuondosha tatizo la kuumia kwa vijana wetu katika mazingira ya viwanja vyetu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli hatujui kwa kiasi gani hivyo vifaa ambavyo tumeviomba vitakuwa ni vya aina gani. Lakini imani yetu itakuwa ni *multipurpose*, vita-*corp* kwenye viwanja vya nyasi na vile vile katika viwanja vyetu. Kwa sababu sisi viwanja vyetu vingi zaidi ni viwanja vya majani ya kawaida na viatu ambavyo mara nyingi huwa tunavitumia kwa kweli ni vya viwanja vya kawaida. Kwa hivyo vikija vya nyasi nafikiri vile vile itakuwa ni bora zaidi. Kwa hivyo nahisi hakuna mashaka na vifaa ambavyo vitakuja vitakuwa ni *multipurpose* kwa viwanja vyote.

Nam. 99

Uundwaji wa Baraza la Vijana Zanzibar

Mhe. Ali Salum Haji – Aliuliza**:-**

Katika kuhakikisha serikali ina nia njema ya kuwaunganisha vijana nchini kote. Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto imo katika harakati za uundwaji wa Baraza la Vijana la Zanzibar.

(a) Je, hatua ya uundaji wa chombo hicho umefikia wapi.

(b) Je, Mhe. Waziri unawaambia nini vijana wa Zanzibar juu ya kukamilika kwa uundwaji wa Baraza hilo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 99 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na mtaalamu muelekezi imeshaandaa rasimu ya awali ya Katiba ya Baraza hilo ambayo ilipitiwa na vijana na kufanyiwa masahihisho. Wizara aidha imeunda kamati ya wataalamu akiwemo mwanasheria kupitia vipengele vyote

vya katiba hiyo ili kuhakikisha kwamba Katiba itakayopatikana itakuwa na muundo mzuri na yenye kuelekeza na yenye kutekelezeka.

(b) Mhe. Spika, nawahakikishia Wajumbe wa Baraza lako tukufu pamoja na vijana kwamba mara itakapokamilika Katiba hiyo Baraza la Taifa la Vijana la Zanzibar litaundwa rasmi.

Nam. 4

Jeshi la Wananchi Kujenga Uhusiano wa Karibu na Wananchi

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza**:-**

Nalipongeza sana Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), mbali na majukumu yake ya msingi lakini pia linatoa huduma za Afya zenye ubora kwa wananchi na zaidi wale walio karibu na kambi mbali mbali za Jeshi hilo. Kambi ya Vitongoji (Ali Khamis Camp) imekuwa mstari wa mbele kutoa huduma za mama na mtoto, kwa zaidi ya asilimia 80% ya wakaazi wa maeneo ya Fidel Castro, Wawi, Furaha na Vitongoji.

(a) Je, ni kwa sababu zipi zilizoipelekea Wizara kushindwa kutoa msaada wa madawa hosipitalini hapo huku ikifahamika kwamba huduma zinazotolewa hapo zinazidi wagonjwa 2000 kwa mwezi.

(b) Kwa vile Jeshi limewapatia nyumba wafanyakazi wawili waliopatiwa na Wizara, ambao ni Mtaalamu wa mama na mtoto na Mtaalamu wa Maabara. Kwa nini Serikali haitoi mwongozo kwa vikosi vya SMZ kuiga mwenendo huo.

(c) Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba huduma bora zinazotolewa hospitalini hapo, usafi, Maabara bora, nidhamu na vitanda kwa wagonjwa, zinatofautiana sana na hali mbaya ya huduma na usafi zinazoikabili hospitali zetu za Mkoani, Wete na Chake Chake.

(d) Kama hivi ni ndivyo, huoni kuwa hii ni aibu kwa Serikali na Wizara iko tayari vipi kuondosha matatizo haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu inayo taarifa ya huduma zitolewazo na Hospitali ya Vitongoji, na jinsi inavyo wasaidia wananchi. Pia tuna ushirikianao wa karibu katika kutoa huduma hizo wapo wafanyakazi wa maabara na watoa huduma kwa akinamama na wajawazito na watoto wachanga ambao ni kutoka Wizara ya Afya. Pia tunawashirikisha wafanyakazi wa Wizara ya Afya waliokuwepo hapo na wale wasiokuwa wa Wizara ya Afya ambao ni wanajeshi tunawashirikisha kwenye Warsha, Semina na Mikutano mengine.

(a) Wizara yangu, haijashindwa kutoa dawa katika Hospitali Vitongoji na hospitali nyengine zote za Vikosi, ila wanapaswa kufuata taratibu za maombi ya dawa hizo, utaratibu ambao ndio unaotumika kwa maombi ya dawa kutoka vituo vyote vya serikali. Mhe. Spika, ila mgao wa dawa kupitia ufadhili wa *DANIDA* hizo haturuhusiwi kuzitumia ila kwa vituo vya afya vya serikali tu.

(b) Mhe. Spika, suala la uongozi wa kuipatia nyumba, wizara kwa ajili ya kukaa wafanyakazi wetu kwa wao walivyofanya ni sawa kwa sababu ni wafanyakazi wetu wamekwenda na wanawahitaji wamewapa nyumba. Lakini mara nyingi vikosi huwa vinafanya kazi kwenye Wizara ya Afya. Lakini litakapotokea suala kama hilo tutazungumza nao ili kuhakikisha kwamba hilo linatendeka.

(c) Mhe. Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi kwamba, Hospitali hiyo ni safi, ina vifaa bora, na huduma zitolewazo ni bora, ubora ambao kwa ujumla unatafautiana sana na Hospitali zetu za Mkoani, Wete, na Chake Chake.

Mhe. Spika, Hospitali ya Vitongoji Jeshini ni mpya kabisa, na imefunguliwa hivi karibuni na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein tarehe 4 Machi, 2011.

Mhe. Spika, Hospitali zetu za Wete, Mkoani na Chake Chake, kimajengo haziwezi kulingana hata kidogo kwa ubora ukilinganisha na hospitali zetu hizo. Hivi sasa, hospitali ambazo zimejengwa zaidi ya miaka 30 iliopita, ndio maana zimekwishachakaa na zinahitaji matengenezo makubwa.

Nafikiri kwamba kwa upande wa nidhamu jeshini na uraiani kuna tofauti, uraiani kuna haki zitimizwe na maadili na jeshini kama jeshi tunavyojua. Kwa hiyo kusema kwamba nidhamu ya jeshi itakuwa sawa sawa na kwetu huku kidogo ni tatizo. Lakini kama haki na wajibu vinatimizwa na maadili yakifuatwa nafikiri nidhamu itapatikana na tunajitahidi kuhakikisha hilo linatendeka.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo juu serikali yetu imeyaona mapungufu yote hayo mapungufu yaliyopo yanarekebishwa. Kwa hiyo hatuoni aibu kwa hilo kwa sababu ndio hali halisi na tutajitahidi kuhakikisha kwamba haki za wafanyakazi wetu zinatimizwa ili wajibu wao unatekelezwa na tuweze kusimamia na maadili waliyonayo.

Lakini hata hivyo serikali inajitahidi kwa misaada ya ICAP, ADB inajenga majumbwa kwa ajili ya wafanyakazi wetu na mahospitali. Tunategemea baada ya muda mahospitali yetu nayo yatakuwa bora.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya nina maswali ya nyongeza mawili madogo sana kama ifuatavyo.

(a) kwa sababu amekiri kwamba hospitali hiyo inatoa huduma nzuri na ambazo zinawasaidia wananchi wetu pia wanapima virusi vya ukimwi lakini hawaruhusiwi kutoa dawa na ushauri nasaha. Naomba kujua ni kwa nini waruhusiwe kupima lakini wasiruhusiwe kutoa dawa na ushauri nasaha.

Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba wanapaswa kuomba dawa kama wanazihitaji ni kwa nini wasiingize katika mpango wa Taifa wa huduma ya dawa na badala yake mpaka waambiwe waombe, wakati kuomba kunaweza kukubaliwa au kukataliwa. Kwa nini wasiingizwe moja kwa moja kwenye mpango wa huduma.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, mimi nashangaa kama wanapima ukimwi bila ya kutoa ushauri nasaha, nafikiri ni kinyume cha maadili. Kwa vyovyote vile iwe kwa hiari, iwe kwa kuolewa iwe kwa lolote lile kwanza unatakiwa upewe ushauri nasaha baadae ndipo umpime mtu virusi vya ukimwi. Mhe. Spika, hilo lina umuhimu wake kumtayarisha yule mtu kuja kukubaliana na majibu yoyote yatakayopatikana liwe ndilo na litakalokuwa silo.

Mhe. Spika, sidhani kama wanafanya hivyo kwa sababu nimempeleka Mkurugenzi wangu kaangalia utaratibu uliopo pale kama wanapima bila ya kutoa ushauri nasaha, bila shaka ushauri nasaha utakuwa unatolewa na tumo katika muendelezo wa kuhakikisha kwamba dawa hapo zinatolewa. Mhe. Spika, ili dawa zitolewe kuna mtiririko wa vitu ambavyo vinatakiwa viwepo, kuna mtiririko wa wafanyakazi ambao wanatakiwa wawepo na pale wafanyakazi hawajakamilika wala hayo mengine yaliyo mepesi ya kutoa dawa pale hayajakamilika. Lakini nia ya kuhakikisha kwamba pale dawa zinatolewa upo kwa sababu wametuomba na tutafanya hivyo.

Mhe. Spika, kuhusu suala la mpango wa dawa nimesema hapa juu kwamba za *DANIDA* ndizo hizo zinazogaiwa kwenye vituo na hizo haziruhusiki kwa makubaliana na Wizara ya Afya na *DANIDA* za serikali na serikali waombe tu wanaomba na wanapewa, asiyeomba sisi hatuwezi tukamfikiria aombe ili apewe.

Mhe. Mbarouk Wadi Mtando: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii nimuulize swali moja la nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Kwa kuwa amekiri kuwa Hospitali za Serikali hasa Mkoani, Wete na Chake Chake kwa ni za muda mrefu na zina uchakavu. Suala hili linalingana na Hospitali ya Kivunge iliyokuweko Mkoa wa Kaskazini.

Je, wizara ina mpango gani wa kusaidia zile nyumba za madaktari ambazo tangu zimejengwa hazijafanyiwa ukarabati na hazina uzio katika eneo lile. Hivyo, serikali ina mpango gani wa kujenga uzio na kuzifanyia ukarabati nyumba zile.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli haya niliyoyasema kwamba hospitali hizi za Pemba na za Unguja ikiwemo Kivunge ni hospitali zilizochakaa na nyumba za wafanyakazi pia zimechakaa. Lakini tumshukuru Mwenyezi Mungu katika mpango wa ADB wa awamu ya tatu tutashughulika na mahospitali mengi makubwa, tutakarabati nyumba, tutakarabati hospitali na tutajenga nyumba nyengine za wafanyakazi ikiwemo Kivunge.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba wizara haijashindwa kutoa dawa katika vituo vyake, lakini atakubaliana na mimi kwamba huko Pemba kuna vituo vingi sana mpaka sasa hivi wameleta maombi ya dawa na mpaka leo hazijafika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, analolisema Mhe. Mwakilishi ni sahihi lakini sio kwamba Wizara ya Afya imeshindwa ila vituo havijapata dawa kwa sababu kuna utaratibu wa kutoka *AMSB* kutoka Bara, pesa zimeshalipwa isipokuwa inategemea *AMSB* je dawa tunaziomba zipo na kama hazipo sisi hatuwezi tena tukenda tukachukua pesa zile tukasema tutanunua dawa nyengine kwengine kwa sababu *DANIDA* wametiliana mkataba na *AMSB* Bara ili kuweza kuleta dawa hizo. Mara tu zitakapofika watatuletea na zinapohitajika zitapelekwa.

Nam. 6

Ujenzi wa barabara sita za kusini pemba

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza**:**

Katika jitihada za Serikali iliyopita chini ya Jemedari wa maendeleo Mhe. Aman Abeid Karume, ilikuwa ni pamoja na ujenzi wa barabara sita za Kusini Pemba, zilizopata ufadhili wa Miradi ya '*NORAD'* ikiwemo barabara ya Mtambile- Mwambe yenye urefu wa 9.4 km.

(a) Ni Kampuni gani iliyopewa jukumu la kujenga barabara hizo sita na barabara zipi zimechukuliwa kama kigezo cha uzoefu na ufanisi wa Kampuni hiyo katika Kanda ya Afrika ya Mashariki.

(b) Ni Kampuni gani inayoleta lami inayotumika kujengea barabara hizo, inatoka nchi gani na ina ubora upi.

(c) Kwa kuwa matuta yaliyowekwa katika barabara ya Mtambile husababisha ajali nyingi badala ya kuzipunguza na matokeo yake yamepelekea vifo vya baadhi ya watu na zaidi ya 15 kulazwa hospitali. Je. Mhe. Waziri huoni kuwa matuta hayo hayakuwekwa kwa kuzingatia ubora wa matuta ya kupunguza ajali.

(d) Kwa kuwa barabara hizo hususan ya Mtambile-Mwambe inaonyesha imejengwa chini ya kiwango, ni lini Serikali itafanya tathmini za awali juu ya barabara hizo ili kujiridhisha na kuchukua hatua zinazofaa dhidi ya Kampuni inayoendelea na ujenzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali lake naomba kutoa maelezo yafuatayo :-

Serikali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipata ufadhili kwa kujenga barabara 6 za vijijini Kusini Pemba kupitia Serikali ya NORWEY.

Barabara hizo ni :-

1. Mtambile - Kengeja, Mwambe yenye urefu wa kilomita 9.4.
2. Mtambile - Kangani yenye urefu wa kilomita 6.4.

3. Mizingani - Wambaa yenye urefu wa kilomita 9.7.
4. Kenya - Chambani yenye urefu wa kilomita 3.2.
5. Chanjamjawiri - Tundauwa yenye urefu wa kilomita 11 na
6. Chanjaani - Pujini yenye urefu wa kilomita 5.

Baraba hizo zinajengwa na Idara ya UUB – Pemba kwa kusaidiana na Mshauri Muwelekezi - Kampuni ya Poyry ya Uswiss. Mradi huu unatekelezwa kwa mfumo wa nguvu kazi (*Labour based*) ambapo wafanyakazi wa vijijini zinapopita barabara hizo hupata ajira na hivyo kutekeleza Sera ya Serikali ya kupunguza umaskini Zanzibar.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 lenye vifungu (a), (b), (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mhe. Spika, hakuna kampuni iliyopewa kujenga barabara hizo. Hata hivyo, ujenzi wa barabara hii ni mpya kwetu lakini umetumika na kupatikana kwa mafanikio makubwa sana kwa nchi ya Afrika ya Kusini na Kenya. Utaratibu huu unapelekea hata ndugu zetu wa Msumbiji na nchi nyengine pamoja na wasomi wa ndani na nje ya nchi kwa masuala ya ukandarasi wa kujenga barabara kuja kwetu hapa Zanzibar ili kuja kujifunza namna uendeshaji na ujenzi wa barabara kwa mfumo huu.

(b) Mhe. Spika, kampuni inayoleta lami hii ni *AL-AFRAD Trading CLC ya Oman* kwa kushirikiana na Kampuni ya Kizalendo ya *Nabeel – Enterprises*. Lami hiyo inatoka Afrika Kusini na Bahrain. Ubora wake unalingana na matakwa ya lami inayotakiwa kutumika katika ujenzi kama ilivyoeleza katika zabuni ya lami hiyo.

(c) Mhe. Spika, matuta yaliyowekwa katika barabara ya Mtambile – Mwambe ni ya muda na yaliwekwa kutokana na maombi au kilio cha wananchi kutoka sehemu iliyopita barabara hii, wakati ambapo ujenzi ulikuwa unaendelea. Hata hivyo, wakati tukiendelea na utiaji lami barabara hii, matuta hayo yamekuwa yakirekebishwa kulingana na ubovu na kiwango kinachohitajika. Aidha, tuna mategemeo ya kuweka alama zote za barabarani ikiwemo zebra na baadhi ya mabango na viashiria vyengine ili kupunguza usumbufu pamoja na kuwa kinga na athari zozote zitakazoweza kusababishwa na matuta hayo kwa watumiaji wa barabara wapya au wageni kwa ajili ya matumizi ya barabara hizo.

(d) Mhe. Spika, sio kweli kuwa barabara hii imejengwa chini ya kiwango na tathmini imekuwa ikifanyika kila muda wa ujenzi unapoendelea.

Mhe. Spia, tathmini ya mwisho iliyofanywa juu ya barabara hii inaonyesha ubora wa hali ya juu ya barabara hii.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, mwaka 2007 Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu ilifanya majaribio ya teknolojia ya romeks katika barabara ya Mgagadu-Kiwani, teknolojia ambayo imefeli na imetia hasara serikali na mwaka huu 2010-2011 teknolojia mpya ya ujenzi wa barabara imeanza katika Jimbo la Kiwani barabara ya Mtambile-Mwambe.

a) Mhe. Spika, naomba kujua tu kuna msukumo gani unaofanya majaribio ya ajabu kufanya kwenye Jimbo la Kiwani na sianze majimbo mengine tukapata kujifunza.

b) Tumegundua kwamba kokoto ambazo zimejengewa barabara hizi zinatoka nje ya Zanzibar ni Tanzania na nyengine kutoka Kenya jambo ambalo kwa mtazamo wangu linaharibu fedha za umma. Ni vigezo gani ambavyo vilipelekea wizara kutoa kokoto Kenya na kuacha kutumia kokoto ambazo zinazalishwa Pemba maeneo ya Mwambe, Micheweni na Vitongoji.

c) Mhe. Spika, mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani na naishi katika maeneo ambayo barabara inajengwa nimeshuhudia na nimesema ni mara ya pili kwamba kinyesi cha ng'ombe kinaondoa lami iliyoko katika barabara ile. Kwa nini Mhe. Waziri akakubaliana na mimi tukaenda moja kwa moja katika eneo hilo ili kumuonesha jinsi vinyesi vinavyochafua barabara ile na mimi ikiwa ni Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani nitaridhika kwamba kuna ubora wa barabara ile na badala yake tubakie kutoa takwimu ambazo mimi siziamini.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, lami iliyofanyiwa majaribio katika njia ya Mgagadu-Kiwani na hii ambayo inatumika katika barabara ya Mtambile-Mwambe ni tofauti kabisa, ile haikuwa lami ilikuwa ni *stabilizing agent* udongo unauchanga na *material* yale ili udongo ule uwe na sifa ya kufanyia barabara. Lami ya huku barabara ya Mwambe-Kengeja hii wanaita *immalger cold mix* ni tofauti mno na hata lami zetu ambazo ni *cold mix*, tumezoea lami za kupikwa na kokoto, hii haipikwi, hii ni *cold mix* unaichanganya na kokoto maalum na ndio maana tukachukua kokoto kutoka Kenya na Tanga. Kwa sababu kokoto za Kenya na Tanga hazinyonyi lami kama zinavyonyonya kokoto zetu za Mwambe na Vitongoji

ambazo zinatokana jiwe la chokaa. Kwa hivyo, namuhakikishia Mheshimiwa kwamba asifananishe vitu ambavyo havifanani, ni vizuri vitu ambavyo havifanani avitofautishe.

Mhe. Spika, ni kwa nini tunatoa kokoto kutoka Tanga au Kenya ni kwasabab hizo nilizozisema kwamba kwa barabara hizi ambazo zunajenga kokote zile ni madhubuti. Lakini tumegundua kwamba kokoto ambazo tunachukua Tanga na Kenya sifa yake ni kubwa, lakini gharama zake ukilinganisha na kokoto ambazo tungezipata pale tofauti yake ni asilimia 15. Hii nasema ni mchakato mkubwa kule tunanunua tunaleta hapa ni kupasua mawe, kuyasaga, tunatumia mafuta, tunatumia umeme, tunatumia vipuri na vitu kama hivyo, ndio maana hatukukaa tu hivi tukasema tuchukue kokoto kule, tumekaa baada ya kufanya mahesabu yetu tukaona kwamba kumbe tungechukua kokoto kutoka Tanga na Mombasa ni gharama nafuu kuliko tungepata kokoto kutoka pale. Kwa hivyo, serikali haipotezi lakini serikali inafanya faida.

Mhe. Spika, chengine ambacho Mhe. Mwakilishi amekisema ni kwamba kinyesi cha ng'ombe kinaondoa lami iliyowekwa katika barabara ya Mwambe-Kengeja na ametaka baada ya kikao hiki au tutafute muda tuende ili akatuoneshe kwamba kweli haya anayosema hapa ni ya uhakika. Nimesema kwamba lami inayotumika barabara ni *cold mix* na mimi siamini mpaka nitakapoona, lakini ninachokwambia Mheshimiwa katika *project* hii ni teknolojia ya kisasa kwa Afrika Mashariki ni Kenya tu ambapo wameanza mradi huu na kwa sababu *project* hii ni ya kwanza na imefanyiwa utafiti wa kina tumefungua website yetu kwa *project* hii tu kwa wale ambao wana mtandao basi wafungue website yetu www.prrp.com waone maoni ya wataalamu all over the world kuhusu mradi huu na ndio maana wenzetu wakashawishika waje waone vipi mradi huu umeweza kutekelezeka huku.

Mhe. Spika, kwa taarifa ya kikao hiki wataalamu wa mradi ule wamealikwa rasmi katika semina au mkutano wa kimataifa unaofadhiliwa na *ILO* utakaofanyika Ghana mwenzi wa Septemba ili waka-present paper na wengine waweze kuuliza maswali na washawishike kuiga teknolojia hii ambayo kwa Afrika ya Mashariki inasema baada ya Kenya ni sisi. Wenzetu wa Tanzania Bara akiwemo Mhe. Magufuli tuna mipango baada ya Bunge aje na wataalamu wake mimi na yeye na wataalamu wangu tuende tukakague barabara hizi kwa sababu zimekuwa na sifa kiasi ambacho amevutika.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mradi huu kama nilivyosema tumeuanzisha sisi Pemba, lakini faida zake ni kubwa. Kwanza imepata uajiri wa wana kijiji ambao barabara inapita katika kijiji chao wameweza kuajiriwa baada ya kufundishwa kwa wiki mbili ni namna gani barabara hizi zinatengenezeka. Kwa hivyo, hata baada ya barabara hizi kufunguliwa na kutumika ni wana kijiji

wenyewe watakaopewa vifaa, watatengeneza wenyewe na bila ya serikali kupata gharama kubwa. Hilo la kwanza.

Mhe. Spika, la pili ni kwamba kilomita moja ya barabara hizi gharama yake ni dola 200,000, lakini barabara iliyojengwa na mkandarasi *MECO, COGEFAR* kilomita moja ya upana huo huo ni kati ya dola 700,000 mpaka dola 900,000. Kwa hivyo kilomita moja ya barabara zinazojengwa na mkandarasi zinajenga kilomita tatu mpaka nne ya barabara za namna hii. Nasema barabara hizi tunazijenga katika vijiji kwa sababu katika vijiji hakuna magari mazito ambayo yataharibu barabara, ni barabara ambazo zinatumika kwa ajili ya matumizi madogo madogo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, sitaki nitumie muda mrefu lakini nawathibitishia kabisa mradi huu ni wa msingi na tukimaliza Pemba tunaelekea Unguja kwa sababu tumewachukua wafanyakazi wa *UUB* kutoka Unguja waende Pemba wamejifunza hadi leo hii wapo na tutaendelea kujenga barabara zetu hizi hazihitaji zana nzito ni zana za kawaida, mikono, majembe lakini barabara ni madhubuti kwa sababu lami inayotumika ni lami tofauti na hii ambayo tumeizoea. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana kunipa ruhusa kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa kuwa serikali ilisema kwamba wananchi wajenge barabara ili kupata ajira, lakini wananchi wale hivi sasa wanapokwenda kutaka kazi huambiwa watowe shilingi elfu thalathini na mwisho wa mwezi hukatwa shilingi elfu tano au siku aliyokuwa hakuja hukatwa shilingi elfu tano na mshahara huo ni shilingi laki moja na nusu.

a) Je, Mhe. Waziri fedha hizo wanazokatwa huwa zinapelekwa wapi.

b) Mhe. Waziri inasemekana kwamba barabara hizo hazitokuwa na ubora hususan barabara ya Mtambile kuelekea Mwambe kutokana na wizi wa vifaa hasa saruji. Je, Mhe. Waziri unalijua hilo na kama utakapolijua una mkakati gani utakayoiweka ili wasimamizi hao wanaosimamia barabara hizo ziendelee kujengwa vizuri na ziwe na ubora wa hali ya juu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli barabara hizi zinatoa ajira ninachokielewa mimi na naona ni hicho hicho ni kwamba kila anayeajiriwa anaajiriwa kwa mkataba na akimaliza kazi yake analipwa shilingi elfu tano. Taarifa ya kwamba wanatoleshwa shilingi

thalathini elfu hii nitaifanyia kazi kwa sababu sina taarifa hiyo, kama kuna mambo yao wenyewe lakini hiyo serikalini haipo baada ya wao kutoa fedha serikali ndio inatoa fedha baada ya kufanya hii kazi.

Vile vile Mhe. Spika, mtu anaponiambia barabara hazina ubora mimi hili nalikataa, barabara zetu sisi tunazijenga baada ya kufanyiwa usanifu na usanifu huu hatwendi kwa mganga, upana wa barabara, umeme wa tabaka za barabara namna ya kukatwa, namna ya kujaza hizi zinatokana na utaalamu hatufanyi sisi usanifu, zinafanywa na kampuni za kigeni kwa mashindano. Kwa hivyo, kampuni ambayo ni bora kuliko zote ndio inapewa kazi hii kwa macho tu hizi ukaniambia kwamba barabara hii sio bora unalinganisha na barabara ipi. Mhe. Spika, hili mimi silikubali, lakini nasema ni barabara na huko tunakokwenda tutaendelea kuziona zaidi.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba wizi wa vifaa mheshimiwa kama kuna mahali ambapo wizi wa vifaa hauwezi kufanyika ni katika ujenzi wa barabara hii, kwa nini nikasema hivyo? Kwa sababu kwanza ujenzi ule una magurupu kila gurupu ni watu 25 siamini kwamba watu 25 wanaweza wakakubaliana waibe saruji mfuko mmoja au miwili na halafu kunakuwa na ukaguzi wa papo kwa papo juu ya hawa wasimamizi. Mhe. Spika, hakuna saruji inayochukuliwa ikawekwa kwa mtu inayobakia inachukuliwa kwenye magari inarejeshwa kwenye *site.* Hili sijui linatokeaje lakini kama nilivyosema inawezekana linatokea lakini mimi siamini kwamba katika mradi huu wizi wa namna hii wa saruji unaweza ukatokea.

Kwa hivyo, ni mambo ya kufanyia kazi tutaendelea kuyafanyia kazi na kila tutakapokwenda tukigundua basi tutatoa taarifa lakini hili la wizi bado hatujaripotiwa na katika mradi kama nilivyosema ambao ni mzuri hauna matatizo kuliko miradi mengine ni mradi wa namna hii. Ndio maana nikasema kwamba tutauendeleza kila mahali, nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, barabara hizi zimepita sehemu kubwa katika Jimbo langu la Mtambile-Mwambe na Mtambile-Kangani yote ni jimbo langu. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Waziri Mhe. Spika, ni kwamba barabara hizi ukifyekuza kwa mguu tu basi lami inatoka kwa hivyo tungemuomba Mhe. Waziri akubaliane na sisi tukamuoneshe humo sehemu mnamotoka hiyo lami, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kama ni maombi mimi nayachukua na tukimaliza kikao hiki basi wale wawakilishi wote ambao barabara hizi zimepita katika majimbo yao na tayari tumeshaanza ujenzi Mwakilishi wa Mtambile, Mwakilishi wa Kiwani, Mwakilishi wa Mkoani kwa

sababu kuna barabara ya Wambaa-Mzingani na hata zile ambazo tumezianza sasa hivi ya Tundauwa na Pujini basi tushirikiane twende tukakague waeleze matatizo yao katika hili na tutalishughulikia Mhe. Spika.

HOJA ZA SERILIKALI

Wizara ya Katiba na Sheria

Mswada wa Sheria ya Mikataba ya Amana ya Mali Zinazohamishika ya 2011

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba Baraza lako tukufu liniruhusu ili Mswada wa Sheria ya Mikataba ya Amana ya Mali Zinazohamishika usomwe kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi mtukufu kwa kutujaalia sote tuliopo hapa kuwa ni wazima na wenye afya njema. Pili naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha mswada huu ambao una lengo muhimu sana la kuwasaidia wananchi wetu na kuwanyanyua kiuchumi.

Mhe. Spika, pia napenda niishukuru Kamati ya Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ali Abdalla Ali kwa kuupitia mswada huu katika kamati kifungu kwa kifungu mpaka mwisho. Nashukuru sana kwamba kamati imefanya marekebisho kwa baadhi ya vifungu kama orodha ya marekebisho iliyotolewa katika Baraza lako tukufu inavyoonesha. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe serikali inakubaliana moja kwa moja na marekebisho hayo kwa maana hiyo Mhe. Spika, naomba mswada huu usomwe pamoja na marekebisho hayo yaliyopendekezwa na Kamati yako ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, mswada una malengo ya kumkomboa mwananchi kiuchumi katika hali yetu ya sasa wananchi wetu wengi ni masikini na hawana mtaji au uwezo wa kujiendeleza kibiashara. Wakati huu mwananchi huyu hana fursa ya mikopo kutokana na masharti magumu yaliyowekwa na vyombo vinavyokopesha. Masharti hayo ni pamoja na kuwa na mali isiyohamishika kama vile shamba au nyumba. Utaratibu huu hautoi fursa kwa wananchi wetu walio wengi kwa kujiendeleza kibiashara na kunyanyua hali zao za kimaisha.

Mhe. Spika, Umoja wa Mataifa katika juhudi zake zile zile za kutaka kuwasaidia wananchi wa nchi zilizo masikini kwa kupitia kamati yake maalum *(United Nations Committee of International Trade Law)* imetoa maelekezo

kwa nchi wanachama kuhusu utaratibu wa kuwanyanyua wananchi wa nchi hizo kwa kuwaruhusu wafanyabiashara wadogo wadogo kuweza kupata mikopo kwa utaratibu mzuri utaowekwa ambao utaruhusu mali ambazo zinahamishika kama vile gari, pikipiki na hata vitu vya dhahabu kuwa ni amana yaani *security* ya mikopo hiyo.

Mhe. Spika, kwa maana hiyo, mswada utawaruhusu wananchi wetu kuchukua mikopo kwa utaratibu utakaowekwa kwa kutumia mfani gari yake mtu, kidani chake cha dhahabu, pikipiki na kadhalika.

Mhe. Spika, mkopo huu anaochukua mtu utakuwa kwa kiwango kile ambacho amana hiyo yaani gari, pikipiki, kidani au chenginecho chochote haitapindukia thamani ya amana yenyewe.

Mhe. Spika, kwa mnasaba huo, katika sheria hii tumezingatia maelezo hayo ya Umoja wa Mataifa lakini kwa kutilia maanani haja na mazingira ya nchi yetu ya Zanzibar. Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba ukopaji huu hauhusiani kabisa kabisa na ukopashaji wa aiana ya rehani ambao ulitumika sana nchini petu katika miaka ya nyuma. Wakati rehani inamfanya mkopaji kufilisiwa mali yake yote aliyoiweka dhamana hata kama thamani ya kitu kile kilichowekwa thamani yake ni kubwa kuliko thamani ya mkopo aliochukua. Mikopo chini ya sheria hii inamfanya mkopaji anaposhindwa kulipa basi dhamana yake itauzwa na fedha iliyopatikana italipia mkopo na kilichobakia atapewa mkopaji mwenyewe.

Faida nyengine ya sheria hii ni kama ifuatavyo:

1. Mikopo itapatikana kwa wingi.
2. Wananchi wengi watanufaika.
3. Wafanyabiashara wadogo wadogo watanufaika sana.
4. Benki nazo zitashawishiwa kutoa mikopo kwa kuchukua dhamana ya mali inayohamishika.

Mhe. Spika, kwa taarifa ya Baraza lako tukufu, wenzetu wa Tanzania Bara sasa wananufaika na mikopo ya aina hii na hata katika vyombo vya kibenki kama vile *CRDB* na *NMB* sasa wanakopesha kwa kukubali dhamana ya mali inayohamishika.

Mhe. Spika, mswada huu umegawika katika sehemu tano, sehemu ya kwanza ina vifungu vitatu vinavyozungumzia jina la mswada wenyewe, tarehe muwafaka ya kuanza kutumika kwa sheria yenyewe pindi ikikubalika, matumizi ya sheria yenyewe ambayo itahusisha mali ya amana iliyopo Zanzibar tu, na hivyo kusimamiwa na sheria za Zanzibar. Vile vile sehemu hii

inatoa ufafanuzi chini ya kifungu cha tatu kwa baadhi ya maneno yaliyotumika katika sheria hiyo.

Mhe. Spika, sehemu ya pili ya mswada huu kunakusudia kuanzisha na kuweka utaratibu mzuri wa masjala ya amana kwa mali zinazohamishika. Kwa mujibu wa kifungu cha nne kutaanzishwa daftari maalum kwa ajili hiyo na mrajis mkuu wa serikali ambaye ndiye atakuwa dhamana wa daftari hilo kwa kuweka au kusajili makubaliano yatayofikiwa baina ya mkopaji na mkopeshaji, pamoja na kuweka kumbukumbu hizo kama kifungu cha sita kinavyohitaji. Mrajis Mkuu wa Serikali chini ya kifungu cha saba anaweza akiwa hajaridhika na maelezo yaliyotolewa kutoka maelezo zaidi au pia kuweka malipo maalum kwa mujibu wa kanuni zinavyoainisha.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu ya mswada huu ina vifungu tisa yaani kifungu cha nane mpaka cha kumi na sita. Sehemu hii inaanzisha haki za amana kwa kuruhusika kisheria kwa mtu kukopa katika chombo cha fedha au kwa mtu binafsi kwa kuweka amana mali yake ambayo inahamishika. Katika makubaliano hayo ni lazima kuwe na taarifa kamili ya mali hiyo pamoja na masharti ya matumizi ya mali hiyo ili mkopeshaji awe ana uhakika wa kupata fedha yake baada ya muda uliowekwa kufika. Kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha mswada ni yule mwenye mali tu ndiye atayeruhusiwa kuiweka dhamana ila pale tu ambapo mali hiyo ipo chini ya udhibiti wa mtu wa tatu ndio mtu huyo wa tatu naye atakuwa na haki ya amana.

Kifungu cha 12 kinafafanua namna ya mali zinavyoweza kutumiwa kama amana. Kifungu cha 13 kinaweka kipaumbele kwa haki ya amana iliyosajiliwa ikilinganishwa na ile isiyosajiliwa. Wakati kifungu cha 14 kinamruhusu mkopeshaji anaweza kupunguza hadhi ya dhamana ya mali ya amana kwa haki nyengine yoyote ile.

Kifungu cha 15 kinatoa fursa ya uhaulishaji wa mali ya amana ila pale ambapo makubaliano yenyewe hayakuruhusu uhaulishaji huo. Kifungu cha mwisho cha sehemu huu kinaelezea utaratibu wa haki ya malipo na namna utavyopewa kipaumbele.

Mhe. Spika, sehemu ya nne inayoanzia kifungu cha 17 mpaka cha 26 inazungumzia namna ya usajili wa makubaliano hayo yatavyokuwa. Usajili huo utafanywa na Mrajis Mkuu wa Serikali ambaye baadae mrajis huyo atawapa wahusika cheti cha usajili, wakati mkopaji akimaliza deni lake basi pia atapewa hati ya utambulisho wa kumaliza deni hilo.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha mswada muda wa makubaliano ya mkopo wa dhamana ni pale tu itapofika tarehe ambayo imesajiliwa kwa

mrajis mkuu kwenye makubaliano hayo. Vile vile haki ya amana pale itapotolewa maelezo basi inaweza kuhamishiwa ikiwa makubaliano hayo ya kuhaulisha yamesajiliwa. Kifungu cha 25 kinaruhusu marekebisho kufanywa kwa makubaliano ya mkopaji na mkopeshaji, na kwamba kifungu cha 26 kinaruhusu daftari la makubaliano hayo kuweza kukaguliwa kwa utaratibu maalum uliowekwa.

Mhe. Spika, sehemu ya tano na ya mwisho inaelezea masharti ya jumla kama vile utumiaji wa jina la amana kwamba halitoathiri masharti ya jumla kama vile utumiaji wa jina, ulazima wa kuwa na nia safi katika makubaliano hayo, haki ya mkopeshaji baada ya mkopeshwaji kushindwa kulipa deni lake au baada ya mkopeshaji kushindwa kutimiza wajibu wake.

Vile vile sehemu hii inampa uwezo waziri anayehusika kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa madhumuni ya sheria hii ikiwemo *fee* ya kulipia makubaliano hayo, mambo yatakayokuwemo ndani ya daftari, taratibu za kukagua daftari hilo pamoja na taarifa nyengine za mali na kadhalika, baada ya mkopeshaji kushindwa kutimiza wajibu wake pamoja na mambo mengine kama hayo.

Mwisho kama kuna makubaliano ya haki za amana yaliyotengenezwa kabla ya sheria basi yataendelea kutumika na kuwa halali kwa kipindi cha miezi sita, baadae ni lazima makubaliano hayo yasajiliwe au vyenginevyo makubaliano hayo hayatakuwa halali kwa mujibu wa sheria hii.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo naomba Waheshimiwa Wajumbe wauchangia mswada huu na baadae kuukubali ili wananchi wetu waweze kujinasua katika hali ngumu ya uchumi, kwa kufanya biashara zao kutokana na mikopo wanayoweza kuipata kutoka benki au kwa watu binafsi kwa kutumia mali zao zinazohamishika.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kuhusu uwasilishaji wa mapendekezo ya marekebisho ya Mswada wa Sheria ya Mikataba ya Amana na Mali zinazohamishika pamoja na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kila sifa njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo hii, ili kuujadili na hatimae kuupitisha Mswada

wa Sheria ya Mikataba ya Amana ya Mali Zinazohamishika. Hivyo, tunamshukuru kwa dhati Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na uhai, afya njema pamoja na taufiki ya kuweza kutimiza wajibu wetu wa kikatiba na maslahi ya wananchi wetu wote.

Mhe. Spika, halkadhalika, napenda kukushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ya awali kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala juu ya mswada uliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala naomba kutoa mkono wa pole kwa Mhe. Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na ndugu na jamaa wa marehemu kufuatia kifo cha Afisa Mdhamini wa wizara hii huko Pemba. Tunamuomba Mwenyenzi Mungu amlaze marehemu mahali pema peponi (AMIN), amuondoshee adhabu za kaburi na sisi tuliobaki atujaalie khatma njema. Aidha, awajaalie wafiwa wote kuwa na moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu, AMIN.

Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kuandaa mswada huu muhimu kwa lengo la kuinua hali ya maisha ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, wakati wa kuupitia na kuuchambua mswada huu katika kamati, nathubutu kusema kuwa kamati yetu ilipata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa watendaji wa Wizara ya Katiba na Sheria, jambo ambalo limeifanya kamati yetu kuweza kufanya kazi hiyo kwa wepesi kabisa.

Mhe. Spika, niruhusu niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mashirikiano makubwa wanayonipa pamoja na michango yao madhubuti wanayoitoa ili kuleta tija zaidi katika Mswada huu. Mhe. Spika, naomba niwatambue kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mussa Khamis Silima	-	Mjumbe
6.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	-	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
8.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
9.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
10.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	-	Katibu

Mhe. Spika, miongoni mwa malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kwamba wananchi wote wanaepukana na umaskini uliokithiri. Katika kutekeleza hili, serikali imeandaa mikakati mbali mbali ikiwemo kuanzishwa kwa Jumuiya za Kiarai, Vikundi vya Ushirika na kadhalika. Aidha, imewajengea mazingira mazuri hata watu binafsi.

Mhe. Spika, kwa kuwa baadhi ya wananchi hawana mali zisizohamishika na kwa kuwa wananchi hawa huhitaji kupata mikopo katika vyombo mbalimbali vya fedha ili waweze kutimiza mahitaji yao ya kila siku. Hivyo, serikali kwa kuliona hili imeamua kuwasilishia Mswada wa Sheria ya Mikataba ya Amana ya Mali Zinazohamishika. Mhe. Spika, hili ni jambo la kupongezwa sana hasa tukizingatia kuwa watu wetu wengi ni masikini wa kipato, lakini ni matajiri wa rasilimali. Hivyo, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanaziendeleza rasilimali zao hizo katika kujikwamua na umasikini walionao ni busara kuwa na sheria ambayo itaweka masharti ya usajili wa mikataba ya amana kwa mali hata zile zinazohamishika.

Mhe. Spika, naomba kuwafahamisha Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa, Mswada huu wa Sheria unaeleza kuwa baada ya mali kusajiliwa mwananchi ataendelea kuitumia mali yake hiyo bila ya usumbufu wowote. Hapa ninamaanisha kusema kuwa, Mswada huu wa Sheria una tofauti na ule utaratibu tuliouzowea wa kuweka rahani. Hata hivyo, kamati yetu inawashauri wananchi kuwa makini baada ya kuweka mali zao katika amana ili kuepuesha mizozo isiyo ya lazima.

Mhe. Spika, kwa kuwa mswada huu tunaoujadili hatimae utakuwa sheria baada ya taratibu zilizowekwa kwenye Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1984 na Kanuni za Baraza la Wawakilishi ya Zanzibar, Toleo la 2011 kukamilika. Kamati yetu inaiomba wizara husika kuhakikisha kuwa wananchi wetu wanapata taaluma ya kutosha kuhusiana na masuala haya ili wasije wakatokezea wajanja na hatimae sheria hii wakaitumia vyenginevyo pamoja na kuondosha migongano ambayo hapo baadae inaweza kutokea.

Baada ya maelezo hayo naomba sasa nije moja kwa moja kwenye mapendekezo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Mikataba ya Amana ya Mali Zinazohamishika. Mhe. Spika, kwenye jina refu *"long title"* kamati yetu imependekeza neno **"**Mswada" kutokana na kuwa sheria yoyote inayotungwa ni lazima kwanza iwe kwenye mfumo wa Mswada ambao hujadiliwa na Baraza la Wawakilishi na baadae Mswada huo kupitishwa kwenye Baraza na kutiwa saini na Mhe. Rais ndio hujulikana kuwa ni Sheria.

Mhe. Spika, kamati ilipendekeza pia, kuongezwe baadhi ya maneno kwenye baadhi ya vifungu ili kuleta maana kamili. Baadhi ya vifungu hivyo ni; Kifungu cha 2(2)(a) Kamati ilipendekeza yaongezwe maneno “ikiwa hazikusajiliwa Zanzibar” baina ya neno “ndege” na “au”, Kifungu cha 3 Kamati ilipendekeza liongezwe neno “kama” baina ya neno “isipokuwa” na “maelezo”. Mhe. Spika, mapendekezo ya marekebisho mengine kama haya ni kama yanavyoonekana kwenye waraka wetu tuliousambaza.

Kamati ilipendekeza pia, baadhi ya maneno yaliyotokana na makosa ya kiuchapaji, baadhi ya maneno hayo ni katika ukurasa wa 90, kifungu cha 2(4) mstari wa kwanza kutoka juu, neno la saba “Makampuni” tumependekeza lisomeke “Kampuni”. Ukurasa wa 94, kifungu cha 13 kwenye maneno ya pembeni neno “Kipaumbile” Kamati ilipendekeza lisomeke “Kipaumbele”. Ukurasa wa 95, kifungu cha 17(4) neno la tatu “mana” tumependekeza lisomeke “amana”.

Mhe. Spika, kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe wamepatiwa waraka wa mapendekezo ya marekebisho ya Mswada husika yaliyofanywa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie marekebisho mengine yaliyopendekezwa na Kamati hii katika waraka huo.

Mhe. Spika, kamati yetu pia imependekeza kufutwa baadhi ya maneno kwenye Mswada wa Kiswahili ili uendane na ule Mswada wa Kiingereza. Baadhi ya marekebisho hayo yaliyopendekezwa ni kama yafuatayo;-

Ukurasa wa 91, kifungu cha 3 kwenye tafsiri ya neno “usajili kuhusiana na haki ya amana”. Aidha, tulipendekeza baadhi ya vifungu kuandikwa upya kutokana na sababu niliyoieleza hapo kabla. Baadhi ya vifungu hivyo ni vifungu vya 8, 24 kwenye maneno ya pembeni vifungu 25(2), 25(3)(c) na kadhalika.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, kamati imependekeza kuongezwa kifungu kipya cha (5) cha kifungu cha 25 ambacho kwa bahati mbaya hakikuandikwa kwenye Mswada wa Kiswahili.

Mhe. Spika, kimsingi huu ndio muhtasari wa kamati kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Mikataba ya Amana ya Mali Zinazohamishika. Nawaomba Wajumbe wote wa Baraza hili wauchangie vizuri mswada huu kwa madhumuni ya kuimarisha zaidi, lakini hatimae kuukubali na kuupitisha bila ya pingamizi yoyote. Baada ya kutamka hayo Mhe. Spika, natamka bayana kuwa mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini na kwa niaba ya wajumbe wangu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, tunaunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha ahsante.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni yangu machache kuhusu mswada huu. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai tukiwa wazima na kupata fursa ya kuchangia.

Mhe. Spika, mswada ni muhimu sana katika kuona kwamba wananchi wanajigomboa katika umasikini na baadhi ya mahitaji ambayo wangepata katika maisha yao, lakini vikwazo vikubwa ni mali isiyohamishika. Sasa hivi tunapata mswada kwamba mikopo inaweza ikatolewa kwa mali zinazohamishika. Pamoja na mswada huu, lakini kuna tahadhari nyingi kabla ya kuendelea ndani zichukuliwe ili mswada huu au mswada utakapopita na kuwa sheria iweze kuwasaidia kwa uhakika na isiweze kutumiwa vibaya na watu wachache.

Mhe. Spika, kwa kuwa utapeli umejaa sana lazima kuchukuliwe hatua za dharura ili anuani kamili za wale ambao wanatiliana mikataba katika mswada huo ziweze kupatikana. Kwa hivyo, kama kuna kifungu ambacho kilisahauliwa cha kupata anuani kamili ya wale wanaotiliana mikataba basi naomba kuangaliwe ni eneo gani ambalo kitaingizwa.

La pili Mhe. Spika, ni suala la makampuni. Kama tunavyoona sasa hivi neno nililotumia hata makampuni yako yanayoundwa kwa utapeli. Kwa hivyo, tunapokuja katika suala la makampuni lazima iwe kuna mtu aliyekuwa ni dhamana wa ile kampuni achukue dhamana ile binafsi asichukue kwa dhamana ya cheo. Kwa sababu gani nikasema hivyo Mhe. Spika? Ni kwa sababu watu wachache watakaoharibu utaratibu mzima huu wa kuchukua dhamana kwa mali inayohamishika wataweza kuwaharibia wengine wengi ambao wao ni waaminifu.

Mabenki yakishapata nafasi ndogo ya kuona kwamba utaratibu huu wa mali zinazohamishika haufanyi kazi kwa kurudisha fedha zao, watakuwa ni wagumu sana wa kutoa na matokeo yake wale ambao wangepata ile nafasi ya kupata mikopo kwa kutumia amana za mali zinazohamishika, basi wataathirika sana. hilo la pili.

Lakini la tatu ni suala la mrajis. Mhe. Spika, utaratibu wetu wa kazi unakwenda kama kwamba kuna kitu unakiomba na sio *formality*. Katika shughuli kama hii ingetarajiwa Ofisi ya Mrajis ikawa na utaratibu wa mpango ambao akifika tu yule mkopaji na mkopeshaji kwa ajili ya mkataba inajulikana anapita njia hii na hii sio mngoje huyu na huyu, kama mambo mengine yanavyokwenda.

Mhe. Spika, unakwenda kwa kushughulikia cheti cha kuzaliwa ambacho ni *formality* kila kitu unacho lakini kuna ucheleweshwaji mkubwa. Sasa mambo kama haya ambayo yule mkopeshaji yeye hana muda wa kukaa pale akakushughulikia, yeye anakwenda pale kama inavyohitaji sheria mwende pamoja. Kwa hivyo, anaweza kusema mimi muda huu siwezi na mkopeshaji akaghairi. Kwa hivyo, Ofisi ya Mrajis inahitaji kujitayarisha na kujipanga kwamba hii shughuli itakapoanza iko tayari kufanya shughuli hiyo au itakuwa ikiwapa tarehe watu kwenda na kurudi na mwisho yule mtu anakosa kile ambacho amekiendea?

Kwa sababu kwa mkopaji ambaye ana mali isiyohamishika anapeleka mkataba tu wa ile mali yake, kama ni nyumba au jambo jengine. Lakini huyu mali inayohamishika inabidi uende kwa mrajis na kukatibiana. Sasa Afisi ya Mrajis ikiwa inaweka watu pale kwa kutaka wawale kwanza halafu ndio wakope jambo hili litakuwa ni gumu sana.

Mhe. Spika, suala jengine ni kiwango cha ukopeshwaji, imetajwa humu katika sheria kwamba itakuwa katika kiwango kile cha mali ambayo imepatikana, lakini kwa soko lipi. Soko la wakati ule au soko linalopanda na kushuka? Kwa hivyo, kiwango hiki kiweze kuangaliwa vizuri ili mali ile itizamwe kutokana na soko liliyopo kwa wakati ule na kwa njia hiyo itabidi Ofisi ya Msajili itayarishe wale watu ambao wanaweka viwango vya soko kwa mali ile.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba mswada huu ni muhimu sana kwa watu wenye uwezo mdogo. Lakini pia usije ukageuka ukawa ni ule wa rahani, kwa yule mtu ambaye atashindwa kulipa na pengine shamba alililoliweka si lake peke yake je, kuna utaratibu gani utakaotumika kuthibitisha kwamba kile alichokiweka ikiwa kimoja ni shamba, kama tunavyojua siku hizi kuna kesi nyingi za ardhi mpaka ikaundwa Mahkama ya Ardhi, kutokana na utaratibu wa sheria hii, kutakuwa na ufuatiliaji wa kiasi gani kujua kwamba shamba ambalo amelitangazia kuliweka amana kwamba ni lake na sio ni mirathi pamoja na watu wengine. Ikiw ani mirathi na watu wengine je, kutakuwa na utaratubu gani wa kuhakikisha kwamba hao wengine wanaitwa na kusikilizwa ridhaa zao. Ni mwepesi kwa kuangalia lakini utekelezaji wake kidogo kwa hasa mambo ya mashamba ni mzito kidogo kutokana na hali ya mabadiliko iliopo sasa hivi.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amepewa nafasi ya kutunga kanuni nyingi tu kwa hivyo namuomba sana aangalie mazingira yote yanayokabiliana na nchi yetu yanayohusu mkopaji na mkopeshwaji, ili kanuni zile zijitosheleze kumpinga yule aliyekopeshwa na kuchukuliwa mali yake, lakini vile vile kumlinda yule mkopeshwaji aweze kupata mali yake kwa wakati.

Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa kwa sababu sheria yenyewe inajieleza na mchango wangu zaidi ulikuwa kwenye tahadhari tu. Isipokuwa nina suala moja tu la mwisho. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akihudhurisha mswada wake alisema benki zitaombwa kutoa mikopo kwa ajili hii ya mali zinazohamishika. Sasa mimi naomba nimuulize kama katika maelezo yake atakuja kutueleza. Baada ya kupita sheria hii kwamba benki itakuwa ni jambo la hiari kukopesha kwa mali inayohamishika au ni *binding* hii sheria kwa mabenki kwamba watawajibika kukubaliana na masharti ya sheria hii ili kukopesha.

Kwa sababu ikiwa hii sheria sio *binding* kwa mabenki bado watabaki na *option* ile ile. Kwa hivyo, mimi nauliza kwamba kwa mujibu wa sheria hiii mabenki ambayo yamo Zanzibar yamesajiliwa au yanafanya kazi Zanzibar kwa mujibu wa hiyo Sheria ya Umoja wa Mataifa iliyokuja na kusaidia. Mabenki yatawajibika kukubaliana na sheria hii au itakuwa kwao ni jambo la hiari na sheria hii sio *binding* kwao.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nakushukuru sana na kwa niaba yangu binafsi na jimbo langu naunga mkono sana hoja hii mia kwa mia kwa vile itawasaidia wananchi. Lakini kabla ya kumaliza natoa tena tahadhari kwamba vipengele vyote vipitiwe ili kuona kwamba isije ikatumiwa vibaya na wananchi wengi baadae wakaja wakakosa hii haki ambayo inawatambalia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi kuweza kuchangia mswada huu japokuwa kwa ufupi tu kwa sababu nilikuwemo katika mswada huu na tumeweza kuuchangia vya kutosha. Kwa hivyo, nataka nitoe maoni yangu kidogo tu.

Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa kuuleta mswada huu ambao leo tunaujadili hapa na mswada huu kwa kweli ukiutazama una haiba kubwa sana kwa wananchi. Serikali siku zote kama ninavyosema kwamba inajaribu kuangalia kila pale penye mapungufu katika maisha ya binadamu basi inakaa tayari kwa kuweza kuwasaidia wananchi wake.

Mhe. Spika, serikali imeliona hilo suala kwamba wananchi wanahitaji kusaidiwa. Hili suala la mikopo halikuanza leo, hata tukitazama katika historia yetu ya zamani tutakuta wazee wetu walikuwa wanakopa kwa matajiri. Hata katika kile kipindi cha uchumaji wa karafuu utakuta wenye mashamba wanakwenda kwa matajiri wanakopa na halafu wanarudisha kwa makubaliano maalum. Hii ilikuwa baina ya mkopaji na mkopeshaji. Kwa hivyo, hili suala si geni kwetu sisi.

Mhe. Naibu Spika, wacha hilo la mashamba hata wake zetu na mama zetu katika miaka ya nyuma walikuwa wanaweka vitu vyao rehani. Kwa mfano, bangili, mikufu ya dhahabu, pete, vitu vyote hivi vilikuwa vinawekwa rehani kwa makubaliano maalum.

Lakini tatizo ambalo serikali imeliona na kwa sababu kulitokezea matatizo katika kukopeshana, ilionekana pale ambapo mwananchi amepeleka vitu kama hivyo na wamewekeana kwa muda maalum na ameshindwa kulipa, tatizo limejitokeza kama kitu tuseme kwa thamani ya shilingi laki tatu na alitakiwa kurudisha kwa wakati maalum na akashindwa kurudisha. Lakini thamani ya chombo kilichokuwa kimetathminiwa ni zaidi ya shilingi laki tatu, lakini yeya kakopa laki tatu. Sasa tatizo ni kwamba pale hasara inampata yule aliyeshindwa kurudisha laki tatu.

Sasa faida inakuwa kwa yule tajiri maana pengine dhahabu zinaweza kuwa thamani yake ni shilingi milioni moja, lakini kwa sababu yeye alikopa shilingi laki tatu ameshindwa kurudisha ina maana faida kwa yule tajiri. Hili serikali imeliona na ikaonekana kwamba kuwe kuna tofauti.

Mhe. Naibu Spika, sisi tunakopa mabenki na tunajua tuna *interest* katika mabenki. Nataka niseme tu kwamba tofauti katika mswada huu baina ya kukopa benki ambayo hapa tunasema atakayeshughulika ni Mrajis Mkuu wa Shughuli za Serikali. Tofauti baina ya Mrajis Mkuu wa Shughuli za Serikali na mabenki ni kwamba kule katika mabenki itaendelea *interest* kama kawaida, lakini kwa Mrajis wa Shughuli za Serikali katika mambo ya kukopeshana huku hakutakuwa na *interest*.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa upande wangu nasema huu umaskini wa muda mrefu uliokithiri serikali imeona ni vyema kuwasaidia wananchi wetu katika kuwakomboa na umaskini huu. Ila serikali imeandaa utaratibu maalum katika kuwasaidia wananchi, hapa tunakubaliana kwa mali ambazo zinaweza kuhamishika. Mali ambazo zinaweza kuhamishika ni nyingi kwa mfano gari ni mali inayoweza kuhamishika unaweza ukaikopea gari ile. Baiskeli ni mali ambayo inaweza kuhamishika unaweza kuikopea na vitu vingi ambavyo mtu anaweza kuvipeleka pahala akakopea.

Lakini sasa kila kitu serikali imeweka utaratibu wake sio tu kwamba mtu atakwenda kukopa zile pesa bila ya kuwa na utaratibu maalum. Kama mtu anataka kukopa gari kwa huyo mtu anayetaka kukopesha ni lazima chombo kile kifanyiwe tathmini kionekane nini thamani ya chombo chake. Kama thamani ya gari tuseme ni shilingi milioni kumi basi yeye katika kukopa kwake haitokuwa milioni kumi ni lazima iteremke chini kwenye milioni sita au saba.

Tunajua suala la magari ni kitu ambacho wewe utaachiliwa mwenyewe, gari utakuwa nayo mwenyewe unaitumia gari yako na gari ile itakuwa una uwezo wa kuikopea chini ya makubaliano ya mkataba maalum baina ya mkopeshaji na mkopaji kwa Mrajis wa Shughuli za Serikali. Huyo ndie atakayekuwa msimamizi mkuu wa shughuli hizi na yeye ndie atakayetoa mkataba huu na tathmini ya vyombo hivyo vitakuwa chini yake yeye kuonekana kwamba hii ndio haki ambayo itatendeka vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini panapokuwa na makubaliano mbele ya mrajis kwamba chombo hichi kimefikia thamani fulani basi itakwenda kwa muda maalum ambao wao wamewekeana. Kwa mfano, yeye amekopa shilingi milioni tano thamani ya gari yake ni milioni kumi, lakini tuseme hatimaye ameshindwa huyu kwa muda ule ambao wamewekeana kuweza kurudisha mkopo ule.

Hapa ukifika muda itabidi kile chombo kiuzwe, kitakapouzwa kwa sababu tathmini ilikwishakufanywa hakutokuwa na hasara, shilingi milioni tano alizzkopa na baada ya thamani ya chombo kitakapouzwa pesa zitakazobakia atarudishiwa mwenyewe. Nafikiri hilo ni jambo zuri na tunawahimiza wananchi wote ambao wenye mali hizi za kuhamishika na wana uwezo wa kupata mikopo wafanyiane mikopo baina ya mtu na mtu na Mrajis wa Shughuli za Serikali ndie atakayesimamia.

Hii yote imeonekana kwamba shida na mahitaji ya watu ni makubwa na uwezo wao wa kupata mahitaji yao ni mdogo, kwa hivyo serikali inawaelekeza watu fanyeni, mkubaliane, mkopeshane na mlipane kwa wakati maalum na mtakaposhindwa basi mtaweza kurejeshewa kile kile baada ya kuuzwa.

Lakini katika yote haya tuseme kitu kikubwa zaidi tunachokifikiria ni hiyo gari. Gari tunavyofahamu sisi inakuwa na sehemu kadhaa wa kadhaa. Kuna *first part risk* na kuna *third part risk* ya chombo. Sasa katika suala hili tunajua *third part risk* mara nyingi ni mtu anapomgonga mtu hapa inakwenda kiserikali ambapo serikali inachukua dhamana. Lakini inapokuwa *first part risk* yaani umei-*insure* ile gari yako katika daraja la kwanza ina maana ile gari itakuwa na hadhi kubwa sana. Kwa hivyo, litakapotokezea lolote katika kusajili ile gari yako au itakapotokezea ajali ya ile gari pale itakwenda kwa mujibu wa *first part risk* haiwezi kwenda kwa *third part risk*. Kwa sababu *third part risk* huwezi kupata kitu.

Kwa hivyo, hayo yote yameonekana na hayo yote katika usajili na mikataba baina ya mtu na mtu haya yatakuwepo jambo hili litasimamiwa vizuri sana.

Mhe. Spika, si baiskeli wala gari tu au vitu vyengine kama tulivyotaja vya nyumbani lakini hata meli tunajua kwamba taratibu meli nyingi zinakuwa zinafanyiwa usajili nje. Lakini tuseme meli iko hapa Zanzibar na kama itasajiliwa hapa kwa makubaliano hayo hayo ya mrajis basi ina maana yule mtu anaweza kupata mkopo ule, chochote kile utakachoweza kukubaliana na mwenzako mnaweza kupata mkopo. Unaweza ukakopa ukapata fedha ile ukatumia kwa haja zako na ukaweza kurudisha fedga ile kwa muda mliowekeana. Itakaposhindikana kwamba umeshindwa kurudisha kwa wakati maalum chombo kile ina maana kuwa lazima kiuzwe.

Mhe. Spika, kwa kweli benki zetu tulizonazo ziko tayari kwa sababu jambo hili si geni kwa Tanzania Bara masuala haya yameshaanza na yanaendelea kama kawaida watu wanakubaliana na mabenki na wanapata mikopo. Sisi mabenki yetu vile vile yako tayari kuweza kusimamia suala hili.

Mhe. Spika, katika masuala haya yatakuwepo masharti ya usajili ambayo hiyo itakuwa ni mikataba maalum ya amana kwa mali zote zile zinazoweza kuhamishika. Hii itamuwezesha mwananchi kuwa na makubaliano vile vile na vyombo vya fedha au pahala popote pale tuseme katika vyombo vya binafsi. Maana yake inaweza kuwa serikalini, inaweza kuwa kwenye mabenki, inaweza kuwa ni mtu binafsi baina ya mtu na mtu.

Mhe. Spika, mimi kwa kweli nilikuwa na hayo tu ya kueleza kidogo na kwamba kwa sababu na mimi mwenyewe nilikuwemo katika mswada huu na mswada huu tumeuchangia vya kutosha na marekebisho kama yale mliyokuwa mmeyaona tumeweza kuyafanya na tumeupitia mswada huu kwa uhakika.

Kwa hivyo, mimi nilikuwa na haya kidogo tu ya kueleza ili wenzetu waweze kuuchangia vizuri bila ya woga, bila ya kuona kwamba labda hizi mali zinazohamishika zitakuwa na ugumu au hazina ugumu. Haya ni mambo ya asili yameanza zamani ila sasa hivi serikali inaweka utaratibu maalum wa kuweza kupata mkopo wa fedha ili kukusaidia katika mambo yako mengine unayotaka kuyafanya.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja hii mia juu ya mia kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Konde. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Mwanaidi Kassim Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia mswada huu. Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo kusimama na mimi kuchangia. Mhe. Spika, pili naishukuru serikali kwa kuleta mswada huu katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, ni ukombozi kwa wanawake, kabla ya mswada huu sheria ilikuwa inawabana sana wanawake ambao wengi wao hawana mali zinazohamishika kama vile nyumba na mashamba. Kwa hivyo, benki ilishindwa kuwakopesha na kuwaamini wanawake.

Mhe. Spika, lakini kwa mswada huu ambao unaruhusu mali zinazohamishika kama vile gari na kadhalika, ni wazi kwamba sheria hii itakuwa ni ukombozi kwa wanawake na wananchi wengine.

Mhe. Spika, jambo la msingi kwa serikali ijiandae vizuri kupunguza urasimu kwa mabenki yetu katika utekelezaji kwa vitendo ili dhamira ya sheria hii iweze kutekelezeka vizuri.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi isipokuwa kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwanza kabisa nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe angalau na mimi kunipatia dakika mbili hizi za kuweza kutoa maoni yangu kuhusiana na mswada ulioko mbele yetu.

Mhe. Spika, pili nadhani nitakuwa mchache wa shukrani kama sikumshukuru Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa ujumla kwa kuweza kufikiria kuleta mswada huu. Mhe. Spika, mswada huu sio tu kama alivyosema mchangiaji mwenzangu aliyepita kwamba umewakomboa wanawake, lakini naweza nikasema kwamba umetukomboa Wazanzibari kwa ujumla bila ya kujali jinsia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mswada huu ni zaidi ya ukombozi kwa wanyonge. Nasema kwamba mswada huu umetuondosha kabisa katika lile jinamizi la rehani ambapo mali zetu wanyonge zilikuwa zinamezwa baada ya kushindwa kurejesha rehani. Mhe. Spika, kwa hili naipongeza sana serikali.

Mhe. Spika, pamoja na pongezi kwa serikali lakini fedha inayotaka kutolewa mkopo ni fedha ya walipakodi wa nchi hii. Lazima umaskini wa hali ya juu uwepo katika kutoa mikopo kwa kutumia hizi *mobile assets*. Ni lazima serikali iwe makini kwa sababu inaweza ikasema kwamba tumeleta mswada huu ili kuwaondoshea madhila Wazanzibari lakini bado ujanja ujanja unaweza ukatokea miongoni mwetu na kuanza kufuja hizi pesa kwa njia hii au nyengine. Kwa sababu hivi sasa zile fedha zilizokuwa zinatolewa katika mfuko wa Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete na Mhe. Amani Abeid Karume zimekwama sana.

Mhe. Spika, hapa unaweza ukatumika ujanja kwa njia nyengine kumeza fedha hizi. Miongoni mwa *mobile assets* Mhe. Spika, ni pamoja na mashua, boti na kadhalika. Sasa serikali pamoja na kufanya tathmini ya mali hizi kwa mfano boti na mmiliki wa boti au mashua akachukua kwa mujibu wa boti yake, ghafla mmiliki huyo akasema boti imezama na ndio aliyochukulia dhamana kule. Boti inaweza kuzama tuseme mathalan lakini je, kama jamaa yangu wa Kojani kaiondosha boti Kojani kaipeleka Mafia hapa ikawa haionekani tena. Sasa mkopaji kama huyu serikali itachukua hatua gani ili fedha zile za walipa kodi ziendelee kuwa salama na zitumike na Wazanzibari wengine.

Mhe. Spika, wakati Mhe. Waziri anawasilisha mswada wake hapa alisema kwamba atashauri mabenki ili kukopesha kwa kutumia hizi *mobile assets.* Nadhani haitakuwa dhambi kwa Mhe. Waziri vile vile kuzishauri hizi Mahkama zetu zikatoa dhamana kwa maana ya *bail* kupitia hizi *mobile assets*. Mhe. Spika, kule Mahkamani hasa sisi wanasiasa tunapokwenda na kesi za kisiasa tunapata tatizo kubwa la kupata dhamana kwa sababu tunaambiwa lazima tuweke *fixed assets*.

Kwa hivyo, tunamuomba sana Mhe. Waziri azinasihi na azishauri Mahkama ziweze kutoa dhamana kupitia hizi hizi *mobile assets.* Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mawazo yangu kidogo katika mswada huu. Mhe. Spika, pili nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala.* Mhe. Spika, tatu nampongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake kwa mswada huu.

Mhe. Spika, huu mswada unavyojionesha kuwa unatutoa katika ule wakati wa zamani ambapo watu walikuwa wakiweka vitu rehani lakini naona ni vile vile tayari tunaweka vitu vyetu rehani. Kwa mfano, nataka kwenda kukopa kwa Mhe. Spika napeleka gari yangu ndio dhamana, sikukulipa Mhe. Spika gari yangu wataiuza, ni ile ile dhamana ya rehani.

Lakini mimi nauliza tu nipate huu ufafanuzi tutakopeshana sisi kwa sisi au kutakuwa na benki maalum Mhe. Waziri ataiweka kuwa sisi tunataka kwenda kukopa pale mrajis atudhamini kwa vile vitu vyetu tulivyonavyo vinavyohamishika tujue. Kwa sababu kidogo mimi huwa napata matatizo juu ya sheria hii ambayo iko mbele yetu, nina tamaa kubwa kwamba itapita katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kutokana na vifungu vyote vilivyomo katika mswada huu, kuna kifungu cha 34(1) kinasomeka kwamba;

Kifungu cha 34(1)

> "Waziri atatunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa madhumuni ya sheria hii".

Mhe. Spika, tuone kwamba sheria hii ni mpya na wananchi wetu wengi hawajawa na uelewa wa mambo kama haya. Kwa hivyo, tungemuomba sana Mhe. Waziri ajaribu baada ya mswada huu kupita kutoa taaluma na kuviwezesha vyombo vya habari kutoa mafunzo kwa wananchi wetu wa Zanzibar, ili waweze kuutumia mfuko huu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Rufai Saidi Rufai. Mhe. Rufai amenikumbusha jambo aliposema kwamba anaunga mkono hoja kuanzia kifungu cha mwanzo mpaka mwisho. Huko nyuma kulikuwa na maelezo ya kukataa hoja kuanzia neno la kwanza mpaka nukta ya mwisho. Kwa hivyo, nakushukuru leo upepo umebadilika sana.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuweza kunipatia nafasi ili kuchangia mswada huu. Mhe. Spika, naunga mkono hoja hi kwa asilimia mia kwa mia, pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Koani, kwamba huu mkopo ni mzuri kwa sisi wanyonge hasa watu wa Jimbo la Koani ambao tupo shamba.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii na kwamba itakuwa nzuri na itatusaidia kwa mikopo yote ambayo inatusaidia sisi wanyonge wa huko vijijini, hasa sisi wengine ambao hatuna gari, lakini tunalo shamba ambalo ni la mboga mboga nafikiri tunaweza hata tukapatia mkopo, ama shamba la mahindi tunaweza kupata mkopo au ufugaji wa ng'ombe wa maziwa au ng'ombe wa kawaida wa nyama tunaweza tukachukua mkopo huo kwa asilimia na kuweza kutanzua matatizo yetu.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri mwenyewe asaidie sana kuwapa mawakala kufika katika majimbo au mashamba yetu ili kupata taaluma maalum jinsi benki hizo zitakuwa wapi au watafuatiwa na benki yenyewe kuweza kwenda kuwapa taaluma wananchi jinsi mikopo hiyo itakavyopatikana.

Mhe. Spika, isiwe mwananchi tu anasema anachukua mkopo, lakini hafahamu chochote wala hana taaluma yoyote. Anakusanya mashamba yote aliyonayo anapeleka mkopo, kumbe vile cha kulipa atakuwa pengine hatopata kuvuna mavuno mzuri itakuwa ni usumbufu. Ni afadhali wananchi wakapata taaluma nzuri mapema kabla ya kupewa huo mkopo na kushirikiwa masheha wa vijijini ili wawape taaluma nzuri.

Mhe. Spika, mimi pamoja na wananchi wenzangu wa Jimbo la Koani tunachoomba zaidi ni kwamba wakati wa mikopo hiyo, basi fedha zitoke kwa fedha taslimu isiwe *cheque aque* kwa sababu wengine hatuna *account* katika mabenki yetu. Kwa hivyo, fedha zitoke bila ya kuwa na *account* yoyote, isiwe zaidi *cheaque* iwe fedha za mkononi ili ziweze kutusaidia kwa mikopo hiyo.

Mhe. Spika, sitokuwa na mchango mkubwa sana, kwa sababu na mimi mwenyewe nilikuwepo katika kuchangia tukiwa kwenye kamati. Kwa hivyo, natoa taaluma tu ya kwamba wananchi wangu wameukubali mswada huu kwa asilimia mia kwa mia uweze kupita, ahsante sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii angalau kutia baraka zangu kwa uchache sana katika mswada huu ambao malengo yake ni mazuri.

Kwanza Mhe. Spika, nataka nianze na madhumuni. Jana nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba madhumuni na sababu za kuletewa mswada ule jana yalikuwa hayajielezi vizuri. Lakini leo niliposoma madhumuni na sababu basi nimejua hasa madhumuni ya kuletwa huu mswada. Kwa sababu hiyo basi nataka nitumie fursa hii kuipongeza sana wizara hii na serikali kwa jumla, kwa kujitahidi kuboresha hali za wananchi. Ni kweli wananchi wetu ni wanyonge na mara nyengine wanashindwa hata pa kuanzia ili wajinasuwe na maisha.

Kwa hivyo, kwa hatua hii inaonekana sasa serikali inawatayarishia wananchi njia ya kujinasua na unyonge, ni jambo la kufurahisha sana. Kwa sababu sisi kama viongozi tupo kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi.

Mhe. Spika, nilikuwa nashauri kwamba hii ni hatua moja nzuri, lakini uzoefu unaonyesha. Kwanza hii sio juhudi ya kwanza kufanywa na serikali, kuna miradi kadhaa huko nyuma imepita na hata juhudi za vikundi fulani vya ushirika vimejaribu sana kutafuta namna ya kunyanyua hali za wananchi, lakini kwa utafiti mdogo niliofanya basi tumefeli sana huko nyuma, kwa sababu ya kufeli ni kwamba wananchi wetu wana taaluma ndogo sana ya kujiendeleza. Kuna miradi imepita, sijui *PADEP*, *TASAF* na vikundi vya mikopo midogo midogo kama hiyo.

Mhe. Spika, mfano anapewa mwananchi kama Shs. 200,000/= au 300,000/=, lakini kwa sababu ya taaluma yake ndogo sana ya namna ya kuzitunza zile na kuziendeleza, basi hatimaye zile pesa zinakwisha na yeye pakushika anakuwa hana na kulipa inakuwa kazi. Kwa hivyo, nilikuwa nashauri sana serikali ichukuwe juhudi za makusudi kwa kutumia njia wanazozijua wenyewe watu wa serikali ili kutoa taaluma ndogo ndogo ambazo zitamuezesha mwananchi

sasa akipata ule mkopo basi aweze kuuendeleza ili apate nafasi ya kulipa na yeye mwenyewe zimsaidie katika maisha yake.

Mhe. Spika, mimi labda nioneshe wasi wasi wangu katika mambo haya ya haki ya amana. Wasi wasi wangu wa kwanza ni namna ya udhibiti wa ile mali ya amana. Kwa sababu najua kwa mujibu wa sheria hii ambayo tunaiandaa, watu wakishakubaliana mkopeshaji na mkopaji, basi hatimaye watakwenda kwa Mrajisi kwenda kusajili mali yake yule atakayekopa. Lakini Mrajis kwake yeye ni kuisajili ile mali, nilikuwa najiuliza je, atakuwa na njia gani ya kuidhibiti ile mali bado iendelee kuwepo na kwa sababu hiyo basi wakati matatizo yakitokea ya ulipaji, basi Mrajis aweze kuwa na namna ya kuipata ile mali. Sasa wasi wasi wangu mmoja ni kuidhibiti ile mali, kwamba Mrajis anaweza kuidhibiti namna gani.

Mhe. Spika, wasi wasi ngu wa pili, ni kwamba mkopaji siku moja mambo yakienda vibaya. Kwa mfano mtu kachukua pikipiki yake kenda kuisajili kwa Mrajis na kama ndio amana yake ya kukopea, lakini mambo yalipokwenda vibaya, basi ule mkopo wa pesa alioupata ukawa umemalizika na haukuleta ufanisi. Je, hatokwepa huyu akaamua siku moja ile pikipiki yake kuiuza kwa mtu mwengine kisha akakimbia, huo ndio wasi wasi wangu. Ingawa nimesoma katika kifungu cha 28 ambacho kinasema pale kwenye kichwa cha habari, haki, wajibu au dhima kufanywa kwa nia safi.

Mhe. Spika, pengine jawabu aliyonayo Mhe. Waziri kwa kuniondoa wasi wasi wangu ni hii nia safi. Lakini nia safi ikiwepo ni sawa, na katika kukopa siku zote mkopaji Mhe. Spika, anakuwa na nia safi, lakini mambo yakimkalia vibaya nia safi inabadilika, anatafuta mbinu ya kukimbia. Sasa sijui kama mpango huu utakuwa endelevu, ndio nikasema kwamba jambo la msingi kabisa ni watu kushauriwa ili waweze kuutumia kwa ufanisi huo mkopo mdogo wanaoupata, kwa sababu Mhe. Spika, mazingira yetu yanaonesha kwamba asilimia ndogo ya pesa katika kiwango hiki, maana hata mtu akiweza kuweka amana baskeli yake au pikipiki basi ni asilimia ndogo sana ya pesa, ambapo kwa mazingira yetu sasa hata *income* yake nayo itakuwa ndogo sana.

Kwa hivyo, mtu kama hakupewa taaluma hasa ya uchumi, basi tutarajie zaidi kwamba atafilisika na hatopata tija. Ndio nikasisitiza sana kwamba jambo la kwanza la msingi kabisa ni wananchi kupewa taaluma ya kwamba akishapata Shs. 400,000/= au Shs. 500,000/= azifanye nini mpaka ziweze kumletea tija na aweze kuurudisha ule mkopo, vyenginevyo utakuwa ni kumtia ndani ya matatizo zaidi.

Mhe. Spika, mswada huu ambao mimi naukubali kwa asilimia mia kwa mia, na nimeusoma sana, lakini ni mswada ambao unahitaji ufundi mkubwa sana

kuweza kuuchangia. Kwa kadiri nilivyovipitia hivi vifungu mimi sikupata la kusema. Labda kifungu cha 29 ambacho kinasema kutekeleza haki ya amana, niliona kidogo labda niseme neno moja katika kifungu hiki, naomba nikinukuu kwanza.

Kifungu cha 29

> "kila mtu atakayehusika na utekelezaji wa haki ya amana, atatekeleza haki yake na kutimiza wajibu wake kwa nia safi na kwa mujibu wa viwango vya kibiashara na hatoweza kujitoa au kwenda kinyume na viwango hivyo".

Sasa hapa kuna maneno, isipokuwa baada ya kushindwa na sio kwenda kinyume kwa mtu yeyote ambaye sio muhusika katika makubaliano. Maneno haya ya mwisho, kuanzia hapo 'isipokuwa' mimi sikuyafahamu, na kwa sababu sikuyafahamu, nilikisoma hiki kifungu mara mbili mpaka tatu mwisho nikayaona hayana maana, ndio nikasema nipendekeze kwa waziri haya maneno labda aje ayafute, au labda aje anifahamishe mpaka niyafahamu vizuri. Lakini kwa hivi ninavyoyaona nahisi kama tukimalizia pale kwenda kinyume na viwango hivyo, basi labda hiki kifungu maneno yakimalizia pale basi kitaleta maana nzuri zaidi kuliko haya yaliyoongezwa.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba mswada huu ni wa kifundi sana na mimi kwa sababu taaluma yangu ya sheria ni ndogo, basi nimeshindwa kupata maneno mengi ya kusema humu. Kwa hivyo, naomba nitamke kwamba naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chonga tunaukubali ahsante.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika mswada huu. Kusema kweli Mhe. Spika, sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kutokana na Mhe. Waziri pamoja na timu yake kuweza kuwasilisha mswada huu kwa namna moja ya nyengine, kama alivyokwishakuzungumza mjumbe aliyepita kuwa uko safi, mzuri na unakidhi haja.

Kwa niaba yangu Mhe. Spika, na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni, napenda kwanza kuchukua nafasi hii kukubali pamoja na kuupitisha mswada huu kwa kuunga mkono kwa asilimia mia kwa mia kutokana na maelekezo ambayo yamekwisha kutolewa. Isipokuwa Mhe. Spika, nina jambo moja ambalo humu nimeliona ningependa kulitolea tahadhari. Mswada huu umepitishwa na umezungumzia namna utaratibu mzima utakavyokuwa unaelekezwa. Isipokuwa katika kipengele hiki cha namna ya ukopaji, hakuna *limitation* hapa.

Mhe. Spika, nimejaribu kuupitia huu mswada na nimeona kwamba hakuna kiwango maalum baina ya mkopaji na mlipaji, ambapo itakuwa wanayo nafasi ya kuweza kucheza hapa. Lakini katika kifungu cha 34, kuna kanuni ambazo zitasimamiwa na waziri. Naomba kwa kuangalia hali za wananchi wetu, kifungu hiki Mhe. Waziri atakapokuja kupitisha mapendekezo hayo ya kanuni kwa ajili ya mswada huu, basi waangalie kipengele hicho na waweze kuwasaidia wale ambao watakuwa wanakwenda kwa ajili ya matatizo haya, hususan watakapokuwa wanakwenda kwa watu binafsi kwa ajili ya shida zao.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja, ahsanteni sana.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuchangia mswada ambao mawazo yake ni mazuri kwa ajili ya kujenga maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, mswada huu unavyoelekea kimawazo ni mzuri, lakini mimi nina wasi wasi kidogo kwamba wananchi tutakuwa tunawapa wazo la kuwa baada ya muda mfupi watakwenda kupata mikopo ya kuweza kujiendeleza. Wasi wasi wangu unakuja kwamba hivi sasa mabenki yetu mengi yana mizigo mikubwa. Sasa mimi nina imani kwamba ile hamu ya kwamba wakopeshe mtu ambaye kenda kuweka baskeli ya Shs. 70,000/= sijui wao watampa ngapi, naona itakuwa ni kama mzigo wa kwenda kusajili kwa ajili ya kumpa mtu Shs. 50,000/=.

Pia watakuwa hawana hamu ya kuona kwamba mtu labda kaweka nyumba ambayo ina thamani kubwa na kashindwa kulipa mkopo au kurudisha mkopo kwa wakati wake, je leo mtu ambaye atakuwa amekwenda kuweka vespa yenye thamani ya Shs. 800,000/= na ambaye anaitumia mwenyewe, wakati wowote inaweza ikapata ajali au ikapata kuibiwa na vyenginevyo. Je, watu hawa watakuwa na imani na mtu huyu tena mkopesha. Kwa hivyo, wazo ni zuri na watu watajenga hamu, lakini nina wasi wasi na utendaji wake kwamba usitusaidie na ukawa haupo.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu ada. Unajua Mhe. Spika, hivi sasa wananchi wengi wamejenga mawazo mengi kwa sababu ada zimekuwa ni nyingi sana. Mfano mtu anakwenda *ZRB* analipa malipo mbali mbali. Labda ningeuliza tu kwamba katika hiki kipengele cha ada atakayelipa ni nani, huyu ambaye atakuwa anakopa. Sasa ikiwa anakwenda kukopa atalipaje ada wakati huyu mtu tayari anakwenda kukopa hizo Shs.50,000/= ada sijui itakuwa ni kiasi gani. Lakini kweli atabebeshwa mzigo mwingine mtu ambaye hana kitu chochote huyu na hii ada itakuwa inakwenda kwa nani. Kwa sababu najenga hoja kwamba ikiwa hii ada itarudia katika mfuko wa Mrajis basi tutajenga mawazo wananchi kwamba tayari serikali imeshaanza njia nyengine ya kujiongezea

pato na sio sisi. Sasa labda ningepata ufafanuzi wa hizi ada zitakuwa zinaingia katika mfuko wa nani.

Jengine Mhe. Spika, ninalotaka kuchangia ni kuhusu, kama mtu ameshindwa kurejesha mkopo au malipo yake, hapa tunasema mali inauzwa. Sasa ikiuzwa kwa njia ya mnada au njia nyengine yoyote ile ili mwenye kukopesha arudishiwe amana yake. Je, hatuoni kwamba tutakapofanya hivi yule ambaye katoa pesa zake kwa muda mrefu kumkopesha yule mtu, leo ile mali ikaja ikauzwa na kuichukua mtu mwengine, hatuone kuwa tutakuwa tunamrudisha nyuma mtu huyu awe hana hamu tena. Kwa sababu kama ni gari anaweza akajenga imani kwamba gari ile ningeipata mimi, lakini tukiitia mnada basi anaweza akatokea mwengine akatia thamani kubwa zaidi. Sasa labda tufikirie uwezekano wa hii kwamba huyu mtu ambaye kakopesha, basi angepewa nafasi kwanza yeye kwamba yaani angepewa kipaumbele ili na hao wengine ambao watakuwa na hamu ya kukopesha waendelee kukopesha.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja hii pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mkoani. Ahsante.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii na mimi kuchangia mswada huu. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kusimama hapa nikiwa katika hali ya uzima na afya.

Pia nachukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri kwa kupitisha mswada huu ambao ni mswada mzuri sana na utaturekebishia mambo mengi tu. Vile vile nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa kupitisha mswada huu katika kifungu hadi kifungu.

Mhe. Spika, mswada huu utatupunguzia kero jingi hususan katika mambo ya mikopo. Mhe. Spika, katika taasisi nyingi ambazo zinatoa mikopo hatimaye hukwama katika vikwazo vya watu wale kurudisha mambo ya mikopo.

Tuchukuwe mfano mmoja Mhe. Spika, wa huu mkopo ambao ulitolewa wa JK na AK, watu wengi kutokana na kuwa hapana utaratibu au sheria ambayo inamgusa mtu basi hatimaye imefika hadi kufika mikopo ile kutokurudishwa kwa kadiri inavyotakiwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mswada huu mimi nadhani kwamba utatusaidia mambo mengi sana. Ninamuomba Mhe. Waziri yeye na wizara yake kuweza kutoa taaluma kwa jamii ambapo na wao waufahamu kwa umakini na kuutambua vizuri.

Mhe. Spika, watu wangi wanapochukua mikopo hudhani kuwa ni pesa ya serikali na huwa haihitaji kulipwa, kwa sababu hawajaona mtu kufungwa kwa

kuwa kachukua mkopo na hakuurejesha. Kwa hivyo, watu wengi hawajali wala hawahisi kitu chochote jambo hili.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi kwa mchango wangu huu naunga mkono mswada huu mimi na walionichangua katika Wilaya ya Micheweni kwa asilimia mia juu ya mia, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi nachukua nafasi hii kukushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu ambao utakuwa ni mfupi sana kwenye mswada huu ambao umewasilishwa asubuhi na Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, kabla sijatoa mchango wangu, kwanza na mimi nitamke kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani.

Mhe. Spika, kwanza kabisa katika mchango naomba niwapongeze Kamati ya Katiba na Sheria kwa jinsi walivyoupitia mswada na kurekebisha maeneo mengi. Vile vile Mhe. Spika, nikupongeze wewe, kwa sababu hata marekebisho yalivyoandikwa yameandikwa kwa taratibu za kisheria na bila shaka hii ni kutokana na kwamba makatibu wa kamati hii ni wanasheria, ndio maana uandishi wao wa marudisho umekuja katika taratibu za kisheria.

Mhe. Spika, katika mswada huu kwa kweli kitu cha kuongezea kikubwa zaidi hatukioni, ila labda tupate ufafanuzi ambao Mhe. Waziri anaweza akatusaidia. Mimi nianzie katika madhumuni na sababu. Katika kifungu cha madhumuni na sababu Mhe. Spika, mswada unasema kwamba umeweka mwanya zaidi kwa wananchi kwamba waweze kuingia makubaliano na vyombo vya fedha.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anifahamishe kuwa katika mswada huu ni jinsi gani mswada umeweka mkakati kwa vyombo vya fedha kuweza kutambua na kudhamini mali ambazo zinahamishika. Wasi wasi wangu Mhe. Spika, ni kwamba pamoja na kuwepo mswada huu, lakini wananchi wanaweza kupeleka vyombo ambavyo vinahamishika kama hizo baskeli na mashua, lakini pengine hao wamiliki wa fedha kwa maana mabenki, wakashindwa kutambua na kuthamini suala hili.

Mhe. Spika, mimi naomba Mhe. Waziri anisaidie, je ni kwa kiasi gani mswada umeweka mikakati kwa vyombo vya fedha kutambua na kuthamini hizi mali ambazo zinahamishika, ili wananchi wetu baadae waweze kupata fursa za kufaidika.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningependa kuchangia ni suala zima la kifungu cha 10. Mimi nipongeze tu kwamba sheria imetambua maslahi ya mtu wa tatu, iwe katika masuala mazima ya mali ya amana. Hili ni suala zuri na kwa kweli Mhe. Waziri hapa nadhani ameipanga sheria hii kwa jinsi ya kutoa haki kwa wahusika wote wa suala hili.

Jengine Mhe. Spika, ambalo ningeomba ufafanuzi ni kwenye kifungu cha 11(3) kuhusu haki amana katika mapato litakuwa halali dhidi ya mtu wa tatu bila ya kujali maelezo ya makubaliano. Mhe. Spika, hapa naomba kidogo Mhe. Waziri anitowe wasi wasi kwa sababu nikiri kwamba mimi sio mwanasheria na mswada huu umeandikwa kisheria mno, kwa hivyo atusaidie katika ufafanuzi.

Aidha, Mhe. Spika, katika kifungu cha 12 Mhe. Waziri anifafanulie zaidi, anisaidie juu ya mali ambazo zisizokamatika na zinazokamatika. Kwa hivyo, naomba kuzijua, kwani kifungu cha 12 (1) kimesema kwamba aina yoyote ya mali inayohamishika, inayokamatika na isiyokamatika.

Kwa maana hiyo, hapa ni vyema tuzijue zipi zinazokamatika na zile zisizokamatika, ili wananchi wetu waweze kujua ni kwa kiasi gani mali zisizokamatika wanaweza kuzikopea siku zijazo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia napenda kupongeza kuhusu kifungu cha 13 kwa kutoa kipaumbele kwa mali ambazo zilizosajiliwa na zile ambazo hazikusajiliwa. Kwa sehemu hii nakuchua fursa hii kuupongeza mswada kwa kuzingatia umuhimu wa mali, ambazo zimesajiliwa kuliko zile ambazo hazijasajiliwa. Kwa kweli hapa napenda kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuweka suala hili wazi.

Baada ya kwenda kwenye vifungu hivyo kwa ufupi nichukue fursa hii kumuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, mambo yafuatayo.

Kwa sababu ya kuondosha urasimu wa kusajili mali ambazo wananchi wamezimiliki zenye kuhamishika, basi nimuombe Mhe. Waziri katika utungaji wa kanuni wazingatie kuhusu suala zima la kuondosha urasimu katika kusajili mali hizi ambazo zinahamishika, ili wananchi baadaye wasipate usumbufu na kuweza kuweka maslahi bora katika mswada huu pamoja na wananchi kwa jumla.

Suala jengine ambalo napenda kumuomba Mhe. Waziri pengine sheria ingeweka wazi, kwamba kuna umuhimu wa kuweka bima kwa zile mali ambazo zinahamishika na kwa zile mali ambazo hazihamishiki kama vile nyumba, ardhi na mambo mengine tayari kuna utaratibu wa kukatiwa bima. Kwa hivyo, sijui kwa mali ambazo zinazohamishika utaratibu utakuwa vipi.

Lakini kuna haja kwa mswada kusema kuwa mali zote ambazo zitasajiliwa zingekuwa na umuhimu wa kukatiwa bima, ili pindipo yanapotokezea majanga kwa mali zile, basi wahusika wote waweze kupata haki zao.

Kwa kweli wasi wasi wangu ni kwamba unaweza kusajili mali na kuikopea na baadaye ikaungua na kama alivyosema Mhe. Mjumbe mmoja hapa, kama mashua ikahamishwa Pemba na kupelekwa Bagamoyo na watu wakala hasara na kuathirika. Sasa kama tungekuwa na utaratibu wa kukata bima katika mali zote ambazo zinahamishika, ili wahusika waweze kupata haki yao pale majanga yanapotokea.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema mwanzo kwamba kamati imemaliza kazi zote na tuone zaidi la kuchangia kwa Baraza. Kwa hivyo, nishukuru kwamba umenipa nafasi na ninaendelea kusema kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja na sote kwa pamoja tuupitishe, ili Mhe. Waziri aweze kuendelea na kazi tukijaaliwa.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba radhi kwa kupoteza muda wako, kwa sababu ya maendeleo ya *technology* kidogo yanatutanza Barazani.

Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima leo kuujadili mswada huu unaoweka utaratibu wa kutumia mali zinazohamishika kama mali ya amana kwa ajili ya kupata mikopo na mambo kama hayo.

Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuchangia mswada huu.

Mhe. Spika, nitangulie kusema kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na mswada huu tayari tumeshautolea maoni kwenye kamati yetu, lakini nimesimama hapa kusema machache pamoja na kuunga mkono mswada huu kwa ukamilifu kabisa. *(Makofi)*

Vile vile nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kama walivyotangulia kusema kwamba tuungane katika kuupitisha.

Mhe. Spika, mswada huu ni mzuri kwa maana nyingi. Kwanza katika kukidhi uandishi mzuri wa kisheria. Pili katika kulinda haki za kila mtu. Kwa kweli kama ilivyozungumzwa hapa kwa muda mrefu tumekuwa na utaratibu

uliozoeleka wa kutumia mali zisizohamishika kama vile nyumba, ardhi kwa ajili ya kuweka amana kwa lengo la kupata mkopo.

Lakini tunajua kwamba asilimia kubwa wananchi wetu ni masikini na wengi hawamiliki vitu kama hivi, vile vile na wao wanahitaji mikopo katika kunyanyua hali zao. Kwa mfano, siku hizi tumekuwa tukitil-ia mkazo sana masuala mazima ya watu kujishughulisha na ujasiriamali, lakini ili uweze kuingia kwenye mkumbo huo, basi unahitaji uwe na nyenzo, fedha ndio nyenzo moja.

Sasa watu wetu hata katika miradi midogo midogo ambayo ingewasaidia kuwatoa pale walipo na kupanda juu kidogo. Kwa hiyo, kuweza kusaidia kunyanyua hali zao za maisha na kupunguza umasikini katika nchi yetu, basi wamekuwa wakipata shida kutokana na kuwa na mali zisizohamishika.

Kwa hivyo, hatua ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba katika Mfumo huu wa Umoja wa Kitaifa kuja na mswada huu. Kwa kweli ni hatua sahihi kabisa katika kuwakomboa wananchi hawa wanyonge, ili na wao waweze kufikia mikopo hii ambayo inatolewa na taasisi mbali mbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jambo la muhimu ni kufahamishana kwamba madhumuni ya mswada huu si kuanzisha Mfuko mpya wa Mkopo, isipokuwa inatumia taasisi ambazo tayari zipo katika nchi zinazotoa mikopo. Lakini unaweka utaratibu, ambapo taasisi hizo ziweze kuwapatia mikopo wale ambao wanazo mali zinazohamishika lakini hawana mali zisizohamishika, ili waweze kuzitumia kwa ajili ya kupata mikopo.

Sasa kama ilivyozungumzwa hapa mswada huu ni mzuri kwa sababu ya mambo mengi. Kwa sababu kwanza unalinda vizuri haki za watu wote, yaani mkopaji na mkopeshaji, kwa sababu huko nyuma kulikuwa na utaratibu katika historia zetu za kuweka mambo kama vile rehani, lakini matatizo yake yalikuwa hayalindi haki ya yule mnyonge, yaani mkopaji.

Kwa mfano, anaweka mali yake na mara nyingi inakuwa na thamani kubwa zaidi kuliko ule mkopo aliopewa, lakini siku akishindwa kulipa mkopo, basi mali yote inafilisiwa, yaani anapoteza kila kitu. Kwa kweli huu umeweka utaratibu kwamba unaweka mali yako kama ni mali ya amana na ukishindwa kulipa mkopo kwa bahati mbaya, basi mali ile itathaminiwa au inauzwa na kukatwa kile ambacho umekikopa na kilichobakia kinarudi kwako. Kwa hivyo, kwa msingi huo unamlinda kabisa yule mnyonge na haki zake zote.

Pamoja na hayo, haulindi mkopaji tu hata mkopeshaji, kwa sababu unaweka utaratibu na mwisho katika sehemu ya tano kuna vifungu vinavyoelezea naomba kunukuu Mhe. Spika.

Vifungu vya 30 na 31 vinasema hivi:-

30 “Haki ya mkopeshaji baada ya mkopaji kushindwa”.

31 “Haki ya mkopaji baada ya mkopeshaji kushindwa”.

Kwa hivyo, tukiangalia tutaona kwamba kuna utaratibu wa jinsi gani ya kumlinda huyu mkopeshaji.

Lakini kwa upande mwengine pia unatoa fursa zaidi mswada huu. Kwa mfano, mali moja unaweza kuitumia kukopea zaidi ya mara moja kwa watu tofauti, jambo la msingi haki zote ziwe zimesajiliwa katika Daftari la Mrajis Mkuu wa Serikali na utaratibu wa kulipa na ikitokezea kushindwa, basi unafuatwa utaratibu wa jinsi zilizovyoandikishwa katika daftari lile na huu ni utaratibu mzuri.

Kwa mfano, ninayo gari thamani yake ni shilingi *million* 10 na nimeitumia katika hatua moja ya kukopea shilingi *million* 3, bado thamani ya shilingi *million* 7 iliyobakia naweza kutumia tena gari ile kwa kukopa sehemu nyengine pengine shilingi million 4 au zaidi. Sasa wakati ninaposhindwa kulipa basi wote watapata haki zao.

Vile vile uzuri wa mswada huu unapatikana katika kuanzisha huu utaratibu wa kuweka hili daftari, yaani *register* pia linasimamiwa na Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali. Kwa hivyo, unawahakikishia wote mkopaji na mkopeshaji kwamba haki zao zitalindwa kupitia Afisi ya Serikali ambayo ndiyo yenye dhamana ya kusimamia haki za wananchi wake.

Mhe. Spika, hayo tukiyatizama kwa ujumla wake yote yanaweka utaratibu mzuri kabisa, unaofanya mswada huu uweze kukidhi mambo mengi yaliyowekwa.

Lakini kwa upande mwengine mswada umezingatia pale mtu anaposhindwa na ndio maana ninauunga mkono, pia ile mali ambayo iliyowekwa mkopo ikatokezewa na janga lolote. Kwa hivyo, imeweka taratibu mzuri kwamba hata zile haki zinazohusiana na mali ile kama vile mambo ya bima na vitu vyengine vinavyohusiana navyo, bado vitamnufaisha yule mkopeshaji kuhakikisha kwamba kile alichokikopesha anakipata kutokana na mambo yale ya bima.

Kwa hivyo, kwa ujumla niseme Mhe. Spika, kwamba mswada huu umezingatia mambo yote ya msingi, ambayo yangepaswa kuwepo katika kulinda haki za wananchi na hiyo ni moja katika *characteristic* sheria nzuri. Kwa maana hiyo, kama nilivyosema mwanzo na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe ambalo wanatoka watu wengi asili yao akiwemo Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Mansoor Yussuf Himid, ambaye ni rafiki yangu, basi sote tunaunga mkono mswada huu. *(Makofi)*

Vile vile nawaomba Waheshimiwa Wajumbe sote wa Baraza la Wawakilishi kupitia kwako Mhe. Spika tuupitishe kwa ajili ya kuweza kutumika, ili uwasaidie wananchi wetu wanyonge kwa kupata mikopo hii na kuweza kunufaika na kujiondoa pale walipo na kusonga mbele zaidi.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nadhani mmetosheka. Kwa hivyo, sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa ajili ya kufanya majumuisho. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kuniruhusu tena kuja mbele ya Baraza hili tukufu kwa ajili ya kujaribu kutoa ufafanuzi kwa yale mambo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyaeleza.

Mhe. Spika, kabla sijafanya hivyo naomba kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote, ambao wamechangia mswada huu na kwa ujumla ni wajumbe 15, ambapo Wajumbe 14 wamechangia kwa kuzungumza katika Baraza lako tukufu na mjumbe mmoja amechangia kwa maandishi.

Kwa hivyo, naomba niwataje wale ambao wamechangia kwa kuzungumza.

1. Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba ya Sheria)
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman;
3. Mhe. Suleiman Hemed Khamis;
4. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa;
5. Mhe. Saleh Nassor Juma;
6. Mhe. Raya Suleiman Hamad;
7. Mhe. Rufai Said Rufai;
8. Mhe. Mussa Ali Hassan;
9. Mhe. Abdalla Juma Abdalla;
10. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa;
11. Mhe. Abdalla Moh'd Ali;
12. Mhe. Bikame Yussuf Hamad;
13. Mhe. Hija Hassan Hija na

14. Mhe. Ismail Jussa Ladhu

Kwa wale waliochangia kwa maandishi ni Mhe. Fatma Mbarouk Said. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wote hao kwa kweli wamekubaliana na mswada wangu, kwa hivyo napenda kuchukua nafasi hii ya kuwashukuru sana kwa mchango wao ambao wameutoa.

Lakini kabla sijaende kwa mchango wa Mheshimiwa Mjumbe mmoja mmoja naomba nisema mambo yafuatayo.

Kwanza Waheshimiwa Wajumbe walikuwa wanataka kuelewa zaidi kuhusu madhumuni hasa ya mswada huu. Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba mswada huu una lengo la kuwanyanyua wananchi wetu ambao kwa kweli hali zao bado ni duni na kipato chao ni cha chini.

Wananchi wetu wanataka kufanyabiashara, lakini kutokana na hali ambayo wanayo hawawezi kufanyabiashara, kwani hawawezi kupata mkopo, kwa sababu mikopo iliopo hivi sasa ni lazima uende benki, wao wanachotaka ni lazima upate dhamana au uwe na kitu ambacho hakihamishiki kama vile ardhi na nyumba. Sasa jambo hili lilikuwa ni gumu kwa wananchi wetu.

Kwa hivyo, mswada huu umejaribu kuyaondoa haya na kufanya kwamba mwananchi ambaye anamiliki mali ambayo inahamishika, basi anaweza kupata mkopo ama kutoka kwa vyombo vya fedha au hata kwa mtu mwengine yeyote ambaye watakubaliana.

Lakini tulisema na ninazidi kusisitiza kwamba mkopo wa aina hii Mhe. Spika haufanani hata kidogo na wala usitafsiriwe kama kuwa ni rehani, yaani ni tofauti kabisa. Kwa kweli mswada huu ukiusoma kwenye vifungu vya 6 na 9 vinaelezea hivyo.

Mhe. Spika, rehani kama tunavyojua wengine wakati wa zamani. Kwa mfano, unacho kidani chako chenye thamani ya shilingi laki 3, sasa unapokwenda kukopa na kukiweka kidani kile na unahitaji kukopa shilingi 50,000/- au 100,000/- sasa unaposhindwa kulipa fedha zile, basi kidani kile kinakuwa si chako tena na kinakuwa cha yule mkopeshaji. Kwa hivyo, fedha zote za juu zilizobakia zinakwenda kwa mkopeshaji.

Kutokana na hali hiyo, ni tofauti na mswada huu, kwa sababu hapa tunasema kwamba ikiwa unayo mali yako ambayo umeiweka katika utaratibu huo. Kwa mfano, unayo gari ambayo umeikopea na thamani ya gari ile ni shilingi milioni 7 lakini ukakopa shilingi milioni 4. Kwa hiyo, unaposhindwa kulipa na gari ile

ikiuzwa, basi kinachotoka hapa ni zile shilingi milioni 4 na zile nyengine zote za juu zilizobakia unapewa wewe mwenyewe. Kwa maana hiyo, hii ndio tofauti kubwa ya rehani na mkopo wa aina hii.

Vile vile kulikuwa na suala la ujumla kwamba ni nani ambao wanaweza kukopo. Kwa kweli ni mtu yeyote anaweza kukopa katika utaratibu huo, pia ikiwa ni kikundi ambacho kimejikusanya na kinacho mali yake ambayo itakubalika, basi kikundi kile kinaweza kukopa.

Mhe. Spika, liliulizwa swali kuhusu wakopeshaji ni vyombo vya fedha ikiwemo benki, lakini hata watu binafsi wanaweza kukopesha kwa utaratibu huu. Jambo la msingi hapa ni makubaliano ambayo mtakubaliana na kwa utaratibu uliowekwa na kupelekwa katika Afisi ya Mrajis, basi hapo panaweza kukopeshwa.

Kwa kweli katika hili naomba nisisitize kitu kimoja muhimu. Mhe. Spika, kuna Mhe. Mjumbe mmoja alisema kwamba sheria hii haikuweka kiwango cha kukopea, ni kweli hatukuweka kiwango cha kukopea. Lakini sisi tulifikiria kwamba hakuna umuhimu huo, kwa sababu kila mtu huruka kwa ubawa wake.

Sasa tukiweka kiwango cha kukopea, inamaana m-*strict* yule mwengine ambaye anaweza kukopa fedha nyingi zaidi. Kwa mfano, mfanyabiashara mmoja anaweza kukopa shilingi 50,000/- kulingana na ile dhamana ambayo anayo, lakini mwengine anaweza kuwa kitu ambacho kinamruhusu kukopa hata shilingi 100,000/-. Kwa hivyo, hii inategemea ile *asset* ambayo unayo na kuiweka kama ni dhamana.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo lilizungumzwa ni kwamba je, vitu hivi ambavyo vinahamishika vikatajwa. Kwa mfano, mashua, gari, pikipiki, vitu hivi vinaweza kuharibika au kupotea ama kuibiwa. Kweli vitu hivi vyote vinaweza kuharibika au kupotea ama kuibiwa.

Lakini tukiangalia katika mswada huu tumesema kwamba Mrajis Mkuu wa Serikali ataweka utaratibu maalum na madhumuni yake ni kwamba lazima kuwe na utaratibu wa kulinda vitu hivi pamoja na kumlinda yule mkopeshwaji, ili aweze kupata fedha zake.

Jambo la muhimu hapa tunaweza kusema ni kufanya *insurance* haina *restrictions*, yaani unaweza kufanya *insurance* ya kitu chochote na pia ziko *insurance* za aina nyingi. Kwa mfano, *insurance* dhidi ya wizi, moto, upotevu, ajali na kadhalika.
Kwa hivyo, Mrajis Mkuu wa Serikali madhumuni yake makubwa ni kuhakikisha kwamba kile kitu ambacho kimekuwa *registered* katika suala hili,

basi kinapata udhibiti mzuri, ili pale mtu ambapo ameshindwa kulipa, iwe kitu kile bado kinaweza kupatikana na kuuzwa na yule mkopeshaji aweze kupata fedha zake.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ya jumla naomba sasa niende kwa ufupi kwa wachangiaji ambao walichangia mswada huu.

Nianze na Mhe. Ali Abdalla Ali ambaye yeye alizungumza kwa niaba ya Kamati ya Katiba ya Sheria namshukuru sana kwa mambo mawili. Kwanza alitupa mkono wa pole kutokana na kifo cha Afisa Mdhamini wetu tunamshukuru na tunamuombea marehemu malazi mema peponi. Pili tunamshukuru kwa ushauri wake ambao ametupa. Kwa hivyo, napenda kumhakikishia kwamba ushauri huo tutauzingatia kama alivyoeleza kwenye maoni yao.

Vile vile suala jengine ambalo alilizungumza ni kuhusu kupatiwa elimu kwa wananchi wetu katika jambo hili. Kwa kweli elimu ni kitu muhimu na hasa kwa sababu suala kama hili bado ni jipya kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, tunahakikisha Mhe. Spika mbele ya Baraza lako tukufu, kwamba tutatoa elimu kwa wananchi katika vyombo ambavyo vinahusika, ili waweze kujua hasa madhumuni yake, utaratibu pamoja na vipi mtu anaweza kupata fursa hiyo.

Mhe. Spika, mchangiaji wa pili alikuwa ni Mhe. Rashid Seif Suleiman ambaye alikuwa anataka kujua anuani kamili kama zitawekwa katika masuala mazima ya mkopaji na mkopeshaji.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mjumbe atizame vifungu vya 6 na 9 ambavyo vinaeleza hasa mambo gani ambayo yanatakiwa katika kuhakikisha kwamba usajili mali ile unakwenda vizuri. Kwa hivyo, kifungu cha 9 kimesisitiza kwamba lazima kuwepo na anuani kamili na maelezo yote yanayohusiana na mali ile na mambo kama hayo.

Sambamba na hilo alisema hizi kampuni nazo zitakuwemo katika utaratibu huu. Mhe. Spika, ninachoweza kusema ni kwamba ikiwa makubaliano yake, kwa sababu ukitizama katika tafsiri kwenye kifungu cha 3 kimeelezea kwamba mkopaji ni nani, anaweza kuwa mtu binafsi mmoja au watu wengi na watu wengi inaweza kuwa ni kikundi fulani ambacho kina lengo fulani na kinahitaji mkopo kwa ajili ya kujiendeleza na shughuli zile.

Pamoja na hayo kama tulivyosema kwamba vikundi hivi ni vile vikundi vidogo vidogo, yaani ni vikundi vya watu wetu ambao ni masikini na hali zao si nzuri. Kwa hivyo, vikundi hivi vidogo hata kama kampuni yao au ushirika wao, basi

haya ndio madhumuni hasa ya kuwasaidia, ili waweze kuondokana na huo umasikini ambao upo hivi sasa.

Kutokana na hali hiyo, si lazima awe mtu mmoja tu, inawezekana ikiwa hata kikundi lakini kwa mujibu wa makubaliano, ambayo lazima wanapokwenda kusajili kwa Mrajis Mkuu wa Serikali, basi utaratibu wote ambao utawekwa baada ya kutungwa kanuni, lazima ufuatwe ili usajili ule uwe na uhakika wa kurejesha zile fedha ambazo mtu amezikopa.

Mhe. Spika, pia Mhe. Mjumbe alizungumzia kiwango cha thamani ambapo suala hili tayari nilishalitolea ufafanuzi na si lazima kiwekwe kiwango cha thamani, kwa sababu inategemea kikundi pengine wengine wanaweza wakataka shilingi 50,000/- na wengine wakataka shilingi 100,000/- na wengine wakataka shilingi milioni 2.

Kwa hivyo, huwezi katika sheria kuweka thamani ama kiwango cha juu au chini cha mkopo, isipokuwa thamani hii inatokana na makubaliano baina ya mkopaji na mkopeshwaji pale, ambapo mtakubaliana na ikiwa ile *asset* au kitu ambacho unakwenda kukiweka itakuwa na thamani ile, basi nafikiri hakutakuwa na matatizo yoyote baada ya kukubaliana na Mrajis Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo liliulizwa na Mhe. Mjumbe kuhusu mkopo huu je unahusiana na mabenki ambayo tunayo na utaratibu wake utakuwa vipi. Ninachoweza kusema kwamba hivi sasa Mhe. Spika kwa wenzetu Bara Benki ya *CRDB* na *NMB* tayari wameshaanza utaratibu huu na tunajua kwamba *CRDB* na *NMB* nazo zina-*operate* Zanzibar. Kwa maana hiyo, ninahakika na kuamini kwamba utaratibu wetu ukeshakukamilika kwamba benki hizi nazo zinaweza kwa haraka kuingia katika mfumo huu.

Ni vyema tujue kwamba benki na vyombo vya fedha ni vyombo vya biashara. Sasa kama ni vyombo vya biashara basi ni lazima utaratibu ukamilike na tuhakikishe kwamba ukopaji huu hautowaingiza wao katika matatizo, ndio maana tukasema kwamba mwanzo itabidi lazima tuweke kanuni na baada ya kuweka kanuni tukubaliane na vyombo hivi, tukeshakubaliana hapo tena baadaye ndipo wananchi wanaweza kuruhusiwa kwenda kwenye zile benki ambazo tutakubaliana nazo.

Kutokana na hali hiyo, naamini *CRDB* na *NMB* watakuwa wamwanzo, vile vile kama nilivyosema mwanzo tutawashawishi na benki nyengine kwa mfano Benki yetu ya *PBZ* pamoja na nyengine, ili na wao waingie katika utaratibu huu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba hivi ni vyombo vya biashara na wao watataka kuhakikisha kwamba kile ambacho watakikopesha, basi lazima kirudi katika mzunguko wa shughuli zao na hiyo ndio tukasema kwamba kutakuwa na utaratibu, ambao utahakikisha kuwa mkopeshaji na mkopeshwaji hawatopata hasara.

Pia lilizungumzwa suala la meli. Kweli tulisema kwamba meli ambazo zinakuwa *registered* hapa ndizo zinazoweza kutumika. Mhe. Spika, jambo hili ni kwa sababu meli na ndege zinakwenda sehemu nyingi, sasa ikiwa kuna utaratibu wa meli hasa meli ambazo kidogo ni kubwa, zinafanya *register* sehemu ambazo ni *convenience*. Kwa hivyo, unapofanya *register* mule basi ile meli inachukua bendera ya mwahala mule na wanaita *flag of convenience*.

Sasa unapotumia meli ambayo ina *flag of convenience* na wala haikuwa *register* hapa na kutumia kwa masuala ya mikopo, basi inaweza kuleta matatizo wakati wa kulipa, ndio maana tukasema katika sheria hii lazima meli na zile ndege ambazo zimekuwa *registerd* Zanzibar ndio zitakazoweza kutumika katika shughuli hiyo.

Mhe. Suleiman Hemed pia aliendelea kuuliza habari ya rehani na mimi namshukuru sana alielezea utaratibu wote na akafafanua zaidi katika masuala ya gari, ambayo yeye alikwenda zaidi na kusema kwamba gari lazima zikatiwe *insurance* ambayo ni *comprehensive* au *full insurance*. Hii ndio itakayohakikisha kwamba linapotokea lolote lile basi yule mkopeshaji anapata pesa zake kama kawaida.

Lakini utaratibu huu Mhe. Spika, kama nilivyosema ni utaratibu ambao utaandaliwa katika kanuni na vile vile utaandaliwa na mrajis Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kwamba mkopeshaji na mkopeshwaji hawapati matatizo katika suala hilo.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa nae namshukuru nakubaliana nae kusema kwamba huu ni ukombozi wa wanawake, lakini pia nafikiri ni ukombozi wa wanaume na zaidi ni ukombozi wa Wazanzibari hasa wale wenye vipato vya chini na ambao wanataka kufanya biashara. Nakubaliana nae kwamba katika suala hili ni lazima tupunguze urasimu na hiyo tutahakikisha kwamba vyombo vyetu vinavyohusika basi urasimu wa aina yoyote ule haupo, ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma hii kwa uharaka unaotakikana.

Mhe. Saleh Nassor nae namshukuru amesema kwamba ukombozi huu ni Wazanzibari wote, lakini yeye alizungumzia kuhusu boti ambalo pia nimeshalielezea kwamba kwa mfano bodi imezama au mashua. Sasa ndio nikasema kabla hayajafanywa mambo haya lazima kuwe na utaratibu maalum

na utaratibu huu utawekwa baina ya mrajis mkuu wa Serikali, ili kujua kwamba yule mtu ambae anakwenda kujisajili katika suala hili la mikopo basi kile kitu ambacho kimesajiliwa kwa kweli hakiwezi kutoroka au kupotea hivi hivi kutokana na utaratibu ambao utawekwa, utaratibu huo uko wa ina nyingi moja wapo ni kuhakikisha kuweka masharti fulani ambayo lazima yatekelezwe.

Ndio maana kifungu cha sita na kifungu cha tisa tumesema wazi kwamba lazima kuwepo na ujuilisho wa kutosha yaani address kamili ya vitu hivi ambavyo vitawekwa katika dhamana.

Mhe. Raya Suleiman Hamad nae alizungumzia kutaka kujua tofauti baina ya rehani na mikopo ya aina hii, pia alitaka kujua kwamba ni vyombo gani ambavyo vitatozwa au vitahusika na mikopo ya aina hii.

Mhe. Spika, nimeshazungumza tofauti baina ya rehani na mikopo ya aina hii na nimeshazungumza kuhusu vyombo ambavyo vinahusika na utoaji wa mikopo hii, vyombo hivyo kama nilivyosema ni pamoja na vyombo vya fedha pamoja na watu binafsi, lakini hasa inategemea makubaliano ambayo yatafanywa baina ya mkopaji na mkopeshwaji.

Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Rufai Said Rufai yeye alikubaliana na mswada huu lakini pia alisema katika kifungu cha 34 basi kanuni lazima ziwekwe vizuri ili kusaidia harakati za shughuli hizi nakubaliana nae, sasa pale ambapo tutatunga kanuni hizi tutahakikisha kwamba *intrest* zote za mkopaji, mkopeshwaji na *interest* ya vile vyombo ambavyo vinahusika basi itatiliwa maanani.

Mhe. Mussa Ali Hassan alizungumzia kuhusu mashamba, hapa napenda niseme tu kwamba utaratibu huu unahusisha mali inayohamishika, kwa hivyo mashamba na nyumba itakua hayamo. Lakini kama kwenye shamba kuna miembe, kuna michenza, kuna mishokishoki ile miti yenyewe ni *fixed* katika ardhi kwa hivyo ile ni miti ambayo haihamishiki. Lakini zile embe, shokishoki, machungwa n.k. vile ni vitu ambavyo vinahamishika, kwa hivyo unaweza kutumia vitu au matunda haya kwenda kukopea katika sehemu hizo ambazo mmekubaliana hiyo ndio tofauti kubwa.

Mhe. Spika, hili suala la kusema fedha ziwe *cash* naomba nitofautiane nae kwamba utaratibu wa siku hizi tunahamasisha kila mtu atumie fedha zake na zitumie benki kwa kunusuru mambo mengi tu, sasa unapokwenda kukopa au ukatoa *cash* pale pale akatoke jambazi itakuwa ameshakutia hasara. Lakini ukienda benk nafikiri inaweza kuwa ni usalama zaidi.

Mhe. Abdalla Juma nae namshukuru ameelezea mengi na amekubaliana na mengi lakini hasa ninachotaka kusema hapa ni kwamba lengo hasa ni kuwanyanyua wananchi wetu, kwa sababu hiyo ndio mswada huu tukaufanya kwamba ni mswada ambao ni rahisi sana kwa wananchi kuweza kuupitia na kuweza kuutekeleza.

Lakini alitaka kujua kifungu cha ishirini na tisa kina maana gani kifungu hiki maana yake kubwa ni suala la namna gani *ile security* iliyowekwa inaweza kutekelezwa na yule aliyekopa, huu ni utaratibu wa kawaida kwamba utekelezaji huu utatekelezwa kwa mujibu wa utaratibu ambao utawekwa pamoja na zile kanuni ambazo zitatunga na kutekelezwa na mrajis mkuu.

Mhe. Mahamoud Moh'd Mussa nae alizungumzia sana kuhusu kiwango cha fedha, lakini nimeshajibu kwamba si muhimu sana kuweka kiwango cha fedha kwa sababu inategemea mtu au makubaliano yale ambayo tumekubaliana.

Pia alizungumzia kifungu cha thalathini na nne ambacho kinazungumzia kanuni nakubaliana nae kwamba katika uandaaji wa kanuni tutakuwa makini zaidi kuhakikisha kwamba yale ambayo yanapaswa kuwekwa basi yanawekwa.

Mhe. Abdalla Moh'd alizungumzia kuhusu vespa na vitu kama hivyo ambavyo wakati unapokopa vitu vile unabakia navyo wewe mwenyewe, lakini baadae vitu vile vinaweza kuibiwa au kupotea sasa je, tutahakikisha vipi kwamba yule mkopeshaji anarejeshewa pesa zake.

Kama nilivyosema mwanzo kwamba kutakuwa na utaratibu maalum ambao utaratibu huo lazima tukae na tuuandae, kwa sababu utaratibu huo ndio utakaochukuliwa na kuhakikishiwa kwamba unafuatwa katika utaratibu wote wa ukopaji.
Mhe. Spika, pia na mshukuru Mhe. Bikame Yussuf Hamad kwa maoni yake na mawaidha yake ambayo ametupa, namhakikishia kwamba tutayafanyia kazi.

Mhe. Hija Hassan Hija nae namshukuru alikubaliana na sisi lakini katika kukubaliana na sisi alisema kwamba angelipenda kupata ufafanuzi kidogo kwa baadhi ya vifungu hasa kifungu cha kumi, yaani haki ya amana kwa mtu hii tunazungumzia mtu wa tatu atakuwa na haki ya amana iwapo tu mali ya amana ipo chini ya udhibiti wake. Hapa tunachozungumzia ni kwamba ile mali ambayo inataka kutumiwa katika kukopa ile ni mali ya yule mtu ambae anataka kukopa ni yake, lakini wakati mwengine mali ile inaweza kuwa kwa mtu mwengine, wewe una mali yako na umemkabidhi mtu mwengine kwa hivyo yeye ni mtu wa tatu lakini si yake lakini kakabidhiwa na kama kakabidhiwa kwa njia moja au nyengine basi ana uhuru au *write* kidogo ya mali ile ni sawa sawa na Mhe. Hija Hassan Hija wewe una ng'ombe wako ukamkabidhi ndugu

yako, sasa yule ndugu yako kama umemkabidhi atakuwa na *write* na anaweza akatumia *write* ile ya kwenda kukopea ndio madhumuni iliyokusudiwa hapa.

Kifungu cha 11(3) nacho kinasema kwamba isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo katika sheria hii haki ya maana katika mapato itakuwa halali dhidi ya mtu wa tatu bila ya kujali maelezo ya makubaliano ya amana yaliyozungumziwa au hayakuzungumziwa mapato. Sasa hii inakuja kwenye kifungu hicho hicho ambacho tunakieleza kwa mifano hiyo, kwamba haki hii inaweza kumrejea kwa yule mtu wa tatu ambae hapa sasa ameshakuwa na haki kidogo katika suala la kukopa.

Lakini kifungu cha kumi na mbil alitaka kujua kuna suala la mali inayokamatika na mali isiyokamatika, zipo mali zinazokamatika na mali isiyokamatika ipo ambayo unaweza kuitumia. Kama tuseme wewe ni mfanya biashara wa *gest* sasa *gest* haikamatiki lakini ni mfanya biashara mkubwa wa *ges*t kwa hivyo ile mali huwezi kuikamata lakini pia unaweza kuitumia katika shughuli hizi.

Mhe. Spika, ninakubaliana na ushauri wake mwengine wa kusema kwamba tupunguze urasimu na namuhakikishia kwamba tutapunguza urasimu katika kutekeleza haya.

Mwisho Mhe. Ismail Jussa Ladhu namshukuru kwa maelezo yake yote aliyozungumza na zaidi ni kutuunga mkono na kusibitisha tu kwamba huu ni mswada mzuri ambao umelenga kumkomboa mwananchi wetu wa kipato cha chini.

Mwisho kabisa napenda nimshukuru Mhe. Fatma Mborouk Said ambae nae alileta maelezo yake kwa maandishi, maoni yake ni kwamba anakubaliana na mswada huu lakini anasema yale yale ambayo yamesisitizwa na watu na waheshimiwa wajumbe wengine kwamba lazima tuwe makini zaidi na katika kuandaa kanuni basi lazima tuziweke vizuri, ili tuhakikishe kwamba walengwa yaani mkopaji na mkopeshaji hawapati matatizo katika suala hili. Napenda nimhakikishie kwamba katika kuandaa kanuni hizo tutafanya hayo kwa maslahi ya mkopeshaji na mkopeshwaji.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo napenda tena niwashukuru waheshimiwa wajumbe wote kwa kuchagia mswada wale ambao wamechangia kwa kusema, wale waliochangia kwa maandishi na wale waliokuwa hawakupata nafasi wote kwa pamoja napenda niwashukuru na kwamba nawaomba tena waukubali mswada huu kwa sababu tukiukubali na kuupitisha basi kwa hatua ya mwanzo tutakuwa tumepiga hatua kuwanyanyua wananchi wetu ambao ni masikini wa

kipato na kuwapa motisha wa kufanya biashara ndogo ndogo ambazo zinaweza kusaidia kimaisha.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi ulioutoa. Sasa niwahoji wale wanaoafiki hoja hii wanyanyue mikono, wasiowafiki wanyanyue mikono. Walioafiki wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Katiba na Shria: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya Baraza zima ili kupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Mikataba ya Amana ya Mali Zinazohamishika 2001

SEHEMU YA KWANZA	-	**UTANGULIZI**
Kifungu cha 1	-	Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu cha 2	-	Matumizi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 3	-	Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake
SEHEMU YA PILI	-	**UANZISHWAJI WA MASJALA YA HAKI ZA AMANA**
Kifungu cha 4	-	Kuanzishwa kwa masjala pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 5	-	Mrajis
Kifungu cha 6	-	Kazi za Mrajis
Kifungu cha 7	-	Uwezo wa Mrajis
SEHEMU YA TATU	-	**KUANZISHA NA KUANZA KWA HAKI YA AMANA**
Kifungu cha 8	-	Haki ya Amana pamoja na marekebisho

Yake
Kifungu cha 9 - Yaliyomo katika bakubaliano ya amana
Kifungu cha 10 - Haki ya amana kwa mtu wa tatu
Kifungu cha 11 - Maelezo ya Mali ya Amana
Kifungu cha 12 - Mali inayotumika kama amana pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 13 - Kipaumbele pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 14 - Kupunguza hadhi ya Mali ya Amana
Kifungu cha 15 - Uhaulishaji wa Mali ya amana pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 16 - Hati ya Malipo ya Umiliki

SEHEMU YA NNE - USAJILI WA MAKUBALIANO YA AMANA

Kifungu cha 17 - Usajili wa Makubaliano ya Amana pamoja Na Marekebisho yake
Kifungu cha 18 - Cheti cha Usajili pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 19 - Hati ya maridhiano pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 20 - Kutambua pamoja na marekebisho hake
Kifungu cha 21 - Uhalali wa usajili pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 22 - Muda wa usajili
Kifungu cha 23 - Kuhaulisha hati ya Amana pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 24 - Kupunguza hadhi Haki ya Amana pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 25 - Marekebisho kusitisha na kumalizika pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 26 - Ukaguzi wa daftari pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA TANO - MASHARTI YA JUMLA

Kifungu cha 27 - Jina la Mali ya Amana pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 28 - Haki Wajibu au Dhima kufanya kwa nia Safi Pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 29 - Kutekeleza Haki ya Amana
Kifungu cha 30 - Haki ya mkopeshaji baada ya mkopaji

		kushindwa
Kifungu cha 31	-	Haki ya mkopeshwaji baada ya mkopeshaji Kushindwa
Kifungu cha 32	-	Utaratibu wa kutekeleza haki pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 33	-	Matokeo ya utekelezaji
Kifungu cha 34	-	Kanuni pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 35	-	Muda wa mpito

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza zima imeuptia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali yote pamoja na masahihisho yake, sasa naomba Baraza lako tukufu liukubali Mswada huu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naukubali.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaoukubali Mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wasiowafiki wanyanyue mikono. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja imekubaliwa na Kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Mikataba ya Amana ya Mali Zinazohamishika 2001

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Mkataba wa Amana ya Mali zinazohamishika 2011 sasa usomwe kwa mara ya pili. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji waheshimiwa wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu katika kusomwa mara ya pili wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja imekubaliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuruni kwa kazi nzuri sana mliyoifanya kuanzia leo asubuhi na tangu jana, shukurani nyengine za pekee ziende kwa Naibu Spika, ambae kwa mara

ya kwanza jana amekalia kiti na kwa bahati ni mara ya kwanza kabisa kufungua mkutano Naibu Spika, na kukalia kiti tangu niwe Spika. Kwa hivyo namshukuru sana ameokoa jahazi na nina taarifa kutoka kwa waheshimiwa wajumbe wengi kwamba kazi ilikwenda vizuri mno.

Kwa hivyo nichukue nafasi hii kukushukuruni kwa kuunga mkono na kushirikiana nae Mhe. Naibu Spika, na ikaenda shughuli yetu hapo jana nzuri sana, sasa kazi nzuri mliyoifanya inamaanisha kwamba bora tupumzike jioni, kwa sababu kazi ya leo tumeimaliza mapema.

(Saa 7.00 Mchana Baraza liliahirishwa Mpaka tarehe 25/03/2011 Saa.300 Asubuhi)